UJUMBE KWA WALIOITWA NA MUNGU

SABABU YA WENGI KUTOKUELEWA BIBLIA, NI KUKOSA KUGUNDUA ILE HALI YA MUUMBA KATIKA HUU UJUMBE WA INJILI YA YESU



Kanisa la kwanza lilikuwa aminifu kuhifadhi Imani lililopewa kwa kizazi chake cha kwanza, lakini baada ya muda, upendo wake ulianza kufifia na, mpango mpya wa kidikteta ukaruhusiwa kukita mizizi, huku, waalimu wapotozao wakiruhusiwa na kuanza kupotoa yale mafundisho ya kweli, na wakaanza kupuuza, yale maagizo kristo aliyowapa mitume.Yesu alikuwa ameonya kuwa, hayo yatatendeka, kama na vile mitume Paulo, na yohana, waliendelea kufanya. Kufikia karne ya pili, ile theologia iliyokuwa ya mitume wa kwanza, ilikuwa imeanza kuongezewa mafundisho ya upotofu kutoka kwa mila za kipagani(Mithira na gnostika). Wakati vitabu vya mwisho vya agano jipya vilikuwa vikimaliziwa kuandikwa, mafundisho ya gnostika yalikuwa yamedhuru kwa kisai kikubwa, yale mafundisho waliyopewa mitume na Kristo. Waumini wengi wa siku hizi hawajui kwamba theologia ya kanisa ya sasa imebadilishwa pakubwa, huku wafuasi wake, wakiyaacha mafundisho yaliyoletwa na Kristo kwa mitume wake.

“Na sasa roho anashuhudia kuwa, wakati wa mwisho, wengine wenu watapotoka na kuiacha Imani, kufuata roho ipotoshayo, yenye mafundisho ya mashetani, huku wakiongea uongo kwa unafiki…….1tim.4:1-2”. Mafundisho ya kimsingi ya kanisa ni saba: **Toba; Imani;ubatizo; kuwekelea mikono; ufufuo; na hukumu ya milele; kila moja yake ikiweka msingi wa kuuendea ukamilifu, kama yanavyoorodheshwa katika Waebrania. 6:1-2.** Sio yote haya ambayo ufundishwa na makundi mengi ya kikristo siku hizi.

KITAMBULISHO.

UUMBAJI NI WA NINI?

Katika anga ambayo haina mwisho, tunajipata katika sayari ya ajabu. Utafiti wa vizazi vingi haujawahi kupata sayari nyingine yenye uhai kama hii yetu. Wanadamu ushangaa ni kwa nini Mungu aliumba dunia peke yake ikiwa na mazingira yanayowezesha uhai uliyo ndani yake. Uhai ulitoka wapi? Je, uhai ni tokeo la kiajali, kama wasemavyo wana evolusheni, au, mpango uliowacha vitu vyote vikihusiana unaachilia ushahidi wa kuwepo kwa muumbaji mwenye hekima ya hali ya juu? Ni kwa nini tuko na huu umbo wa kimwili?

KWA NINI ADAMU ALITENDA DHAMBI?

Yule mtu anayetajwa katika Mwanzo, kama mtu wa kwanza, aliumbwa kutoka kwa mavumbi ya ardhi, na kufanywa kiumbe hai kwa kupuliziwa pumzi ya Mungu. Aliumbwa akiwa hana ufahamu, lakini akapewa uwezo wa kupokea ufahamu katika hiyo hali, ila pia, alipewa, uhuru wa kuchagua.Kujua na kutembea na Mungu kama alivyoagizwa, na hata hivyo, kuchagua kuasi,ni swali tunaloliuliza; ni kwanini alichagua kuasi? Hatuelezwi ni muda gani Adamu na Awa walimtii Mungu kabla hawajaasi, lakini tujualo ni kwamba, waliasi na kuondolewa kwenye Bustani. Baada ya uasi, walikuwa waanzilishi wa vizazi vilivyofuata, ambavyo walivifundisha uasi, huku wote wakijiletea hukumu ya kifo. Wote watakaoendelea na maisha aliyoyaanzisha Adamu, watakufa. Swali kubwa basi ni hili: ni kwa njia gani, wanadamu wataweza kuepukana na hii hali? Ni kitu gani Mungu alifanya,kubadilisha hii hali ya kufa?

SIRI YA UTAUWA YAFUNULIWA;

Mwanadamu hakuumbwa wa kuishi muda mfupi tu halafu hapatikane na gadhabu ya Mungu, huku akiadhibiwa vikali milele, au kuangamia kabisa.Hata hivyo, hii ndio hukumu kwa wale watakaobaki kwenye haya maisha aliyoyaanzisha Adamu. Kunao sababu kuu ya mwanadamu kuwepo hapa duniani, ambayo wengi wetu hawaifahamu. Kristo Yesu alikuja kufunua hiyo sababu, mpango mkuu waliokuwa nao, yeye na baba Mungu, hata kabla kuumbwa dunia.Lakini huu mpango umefichika kwa wengi, isipokuwa wachache ambao Mungu amekusudia kuwaita katika hiki kizazi. Hata hivyo, kunao wakati ambao, kila apendaye, ataweza kujikabidhi kwa huu mpango wa Kristo wa msamaha.

MWANADAMU ALIUMBWA KWA MPANGO MKUU;

Katika ujumbe wa ufalme wa Mungu, kunao maelezo ya kusudi la kuumbwa kwa mwanadamu.Dini zimepuuza haya maelezo ambayo yako katika injili ya Kristo. Ijapokuwa

wanakubali kufanyika kwa wanadamu kuwa wana wa Mungu, kwa njia ya kuongoka, mengi ya vile hiyo itafanyika hawayafundishi. Yesu mwenyewe anaumba wanadamu ambao atashiriki nao katika jamii ya baba Mungu milele. Kwa sasa, ni wachache wanaitwa, huku wengine wakiitwa baadaye. Mwanadamu anao uwezo wa kupokea roho ya Mungu baada ya kutubu, na kubatizwa, na kuwa na hali halisi ya Mungu ndani yake. Kwa huyo roho, mwanadamu anaweza kuumbika sura ya Mungu, na hata mwisho mwisho, kuwa na mwili kama wake. Wakati Kristo atakapokuja, wateule wake wote watafufuka wakiwa na hiyo miili ya kiroho. Ni kusudi lake Mungu kwamba, wote aliowaita waweze kushiriki huo utukufu wake. Hiyo roho yake ndiyo ule uwezo tuanotumia kuumbika tabia yake ya uhaki ndani yetu.Wale watakaofaulu kuumbika kikamilivu, watapewa mamlaka juu ya mataifa.Watakuwa watawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu moja. Ni dini chache zinazofundisha hayo siku hizi.

UTANGULIZI

Kwa maneno yake mwenyewe, Yesu Kristo alisema kuwa alikuja kutangaza, **kuja kwa ufalme wa Mungu.** " Baada ya yohana kutiwa gerezani, Yesu alikuja Galilaya akifundisha kuhusu ufalme wa Mungu, akisema, 'wakati umewadia na ufalme wa Mungu ukaribu; tubuni, mkiamini injili-Marko.1:14-15". Akawaambia, " imenipasa pia kufundisha ufalme wa Mungu kwa miji mingine pia; maana ni kwa sababu hiyo nalitumwa-Luka 4:43". Hata ikawa baadaye, alienda kwa kila mji akifundisha habari za ufalme wa Mungu, na wale kumi na wawili walikuwa naye-Luka.8:1. Hivi, na vifungu vingine vingi vinaonyesha kusudi la ujumbe wa Yesu kuwa, tangazo la kuja kwa ufalme wa Mungu. Je, dini za wakati huu zinaeleza vile huu ufalme utakavyokua? Pia, kusudi la Yesu ilikuwa kwamba, kila ausikiaye huu ujumbe auelewe? Kwa kufikiria kwetu, tunaweza kusema ndio.Kunao maelezo yanayothibitisha kwamba, huu ujumbe ulikusudiwa kwa wachache, wakati huu, na sio kila mtu. " akawaambia, hii siri ya ufalme wa Mungu imepeanwa kwenu tu kuijua, hila kwa wengine, ni kwa mafumbo, ili kuona wasione, na kusikia wasisikie, wala kuelewa-Luka.8:10. Ni wazi kwamba, mafumbo ni ya kuwafanya wale hawajachaguliwa wakati huu, wasielewe. Soma pia- Mat.13:10,13,34,35. Ni wale tu ambao wamepewa kuelewa, wale ambao baba amewachagua na kuwapa roho yake, ndio watakaoelewa katika kizazi hiki cha leo. Tunatakiwa kuelewa pia, ujumbe wa yesu ulikuwa na mambo mapya ambayo wale wafuatao agano la kale peke yake, hawawezi kuyaelewa. Tunaambiwa, " torati na manabii zilikuwa mpaka wakati wa yohana. Tangu hapo, ufalme wa Mungu unahubiriwa, na wanaoutafuta uuendea kwa nguvu- Luka 16:16". Hiki kitabu kimekusudiwa kuwaelimisha wale, ambao kwa uhakika wanataka kufahamu injili ya Yesu, na kuelewa kusudi la Mungu la kuiumba Dunia, na kusudi la mwanadamu. Ufalme wa Mungu haujawahi kueleweka vyema na wengi. Maelezo utolewa, lakini uelewa mkamilifu utapatikana kwa vifungu vya biblia. Tunaagizwa, "…. Kuutafuta kwanza ufalme wa Mungu na uhaki wake, na hivi vingine vitatufuata-Mat.6:33". Pia, "Jitahidi kujionyesha kuwa anayekubalika na Mungu, huku ukiitumia kwa halali, neno la kweli-2Tim.2:15". Kwa nini tunahitajika kubadili mienendo yetu, na kuwa watiivu kwa amri za Mungu, kama vile Yesu alivyofanya, ikiwa hazileti tofauti yeyote? Yesu anasema, 'amini, amini nawaambieni, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme

wa Mungu……mtu asipozaliwa kwa maji na roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu-john.3:3,5". Hii ni kufuatana na kubatizwa na kupokea roho ya Mungu.

YALIYOMO

Mungu Amefunua Mpango Wake Kuhusu watu Wote

Anathihirisha Ile Hali ya ujumbe Wa Inili

1:Kunao kusudi kuu inayofunuliwa kwa wanadamu……..Ukr 1

a) Uhai kama tuujuavyo ni kitu cha ajabu katika hii anga letu

b) Mungu anaumba jamii iliyo kama yeye

c) Kristo atatawala dunia yote kwa muda wa miaka elfu moja

d) wateule wake watatawala pamoja naye kama wafalme na makuhani

e) Mteule ni mtu wa aina gani?

f) Huo ulimwengu ujao ndio ufalme wa Mungu wa kweli

g) Sabato ya siku ya saba ni onyesho ya huo mpango

h) Sikukuu zilizoorodheshwa kwa biblia pia uonyesha huo mpango kwa undani Zaidi

i) sikukuu za kawaida za madhehebu usheherekea uongo

2: wote wanakusudiwa kuitwa na Mungu kwa wakati wake……..Ukr.4

a) Wachache tu ndio wameitwa kwa wokovu wakati huu
b) Wengi hawajaitwa wakati huu
c) Wengine wamepofushwa makusudi
d) Kunao nyakati mbili za mavuno
e) Kuitwa uanzisha uhusiano wa upendo kwa Mungu na, kwa wandugu
f) Shetani atafungwa wakati wa mavuono ya pili

3: Amri za Mungu ni msimamo wa milele……..,…..Ukr.6

a) Amri za Mungu ni maelezo ya utakatifu wa kweli

b) Ukristo wa kimila unapuuza utiivu wa amri za mungu

c) Kristo hakuondoa amri za Mungu wala manabii

d) Alizitimiza kama kielelezo kwetu, ili tufanye kama yeye

e) Kuvunja hizi amri ni dhambi na uleta kifo

f) Nehema uchangia kuondolewa kwa dhambi, lakini sio ruhusa ya kuendelea kusini

4: Umuhimu wa maagano……..Ukr.7

a)agano utoa habari kwa mtu

b) Agano ni makubaliano kati ya wawili

c) ubatizo ndio thibitisho na mwanzo wa uhusiano wa mtu na Mungu

d) Kuwacha makubaliano ya mtu na Mungu uleta kifo cha milele

e) agano jipya imejengwa juu ya amri za Mungu

f) Agano la kale ilifundisha maadili ya haki kwa watu wasioongoka

5: Kuongoka kwa kweli ni hali isioeleweka na wengi……..Ukr.9

a)Kwa nini watu wote wanahitaji wokovu?

b) wokovu na msamaha wa dhambi ni kipawa cha bure

c) Kuongoka ni maisha ya kupigana huku mtu akishinda mpaka mwisho

d) Tunatuzwa kulingana na matendo yetu

e) Imani, toba, na ubatizo zinahitajika kabla mtu kupokea roho takatifu

f) Bila roho takatifu, mwanadamu hajiwezi

6: Kutakuweko na Ufufuo wa wote ambao wamewahi kuishi……..Ukr.11

a)wateule wote watafufuka wakiwa na kutokuharibika, yesu ajapo mara ya pili

b) Kutakuwa na sherehe ya kutuzwa siku hiyo ya ujio wa pili

c) Idadi kubwa ya wafu watafufuliwa baada ya miaka elfu moja

d) Kunao nafasi bado ya wale waliokufa kabla hawajaitwa

e) watakaokana wokovu watakuwa wamejipatia kifo cha pili

7: Kifo cha huu mwili ni kama hali ya kulala kwa muda…….ukr.12

a)Kifo cha huu mwili sio cha milele

b) Mwili huu wa nyama sio wa kutokufa

c) Hakuna ufahamu katika mauti

d) Kifo cha pili ndicho mwisho wa wenye dhambi

e) Kitakuwa ni kwenye ziwa la moto

8: Hukumu ya walio wengi na baada ya utawala wa miaka elfu……ukr.13

a)Ni wale tu ambao wameitwa saa hii ambao wanahukumiwa sasa

b) Wengine wataanza hukumu yao hapo Yesu ajapo mara ya pili

c) Hukumu ya haki ni lazima ihuzishe kufunuliwa kwa matendo yote

d) Huku kufunuliwa kwa matendo ndiko kunaachilia uamusi

e) Adhabu ya milele-mauti ya pili- ni ya haki, nay a mwisho

Ni nani farasi Mweupe Katika Kitabu Cha Ufunuo?

Ijapokua wengi wa wahubiri ufundisha kuwa, farasi mweupe wa ufunuo 6 ni Yesu, uchunguzi wa makini wa unabii alioutoa Yesu akiwa mlima mzeituni katika Mathayo.24(marko.13), unaonyehsa waziwazi kuwa huu ufunuo 6 unaachilia Kristo wa uongo ambaye atawadanganya wengi.

Mathayo.24:4-6. " Yesu akajibu na kuwaambia, ' angalieni mtu asiwapotoshe.Maana wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, ndimi Kristo, na watawapotosha wengi".

Ufunuo.6:1-2. " Basi nikatazama, mwanakondoo alipoufungua muhuri wa saba, nikasikia mmoja wa wale viumbe wane walio hai, akisema kwa sauti kama gurumo, " njoo!" Nikaangalia, na tazama, Farasi mweupe! Na aliyeipanda alikuwa na uta mkononi, na akapewa taji, akatoka kwenda kupigana na kupiga".

Ndio, wanaopigwa hapa ni wanadamu. Hii ndio maana kamili la jina, NIKOLAITANI! Ule mpango ambao Kristo anasema, anauchukia(ufu.2:6,15). Hapa, Kristo anawaonya mitume na pia wote waaminio, kujihadhari, wasije wakapotoshwa, na wahubiri wa injili ya uongo ambayo itajiri. Ni kweli Kristo anaonyeshwa akipanda Farasi mweupe, akirudi duniani kutawala(Ufu.19:11-16), lakini huyu Farasi mweupe wa Ufu 6 si yeye, maana yeye haji kwa uta ila kwa upanga ambao ni neno la Mungu. Huyu mpandaji hii farasi anaonyeshwa akiwapotosha watu, na atajionyesha kama kristo, au, anayemwakilisha Kristo, huku akiingiza injili yake ya uongo, ambayo anaita ukristo. Huyu mpandaji atakuwa kiongozi wa dini, anayepigana akijificha kwenye chapa ya utauwa. Huu uta unaonyesha uwezo wake wa kutumia majeshi ya wanadamu, kutimiza lengo lake, huku hilo taji likiwakilisha utawala wake, na kweli, atatawala. Hii ndio hali iliopo katika ulimwengu wa sasa.

Mashahidi wawili wa mwisho, kabla ya mwisho wa wakati

Ufunuo.11:1. "Na nikapewa, kijiti kama fimbo:na malaika akasimama na kuniambia, ' simama upime hekalu la Mungu, na madhabahu, na wale wauminio ndani.

2: Lakini sehemu ya nje la hekalu, usipime; maana wamepewa mataifa, na wataukanyanga huu mji mtakatifu, kwa miezi arobaini na mbili.

3: Na nitawapa uwezo, hawa mashahidi wangu wawili, ili watabiri kwa muda wa siku elfu mbili mia mbili na thelathini na sita, huku wamevalia magunia.

4:Hawa ndio ile mizeituni miwili, na ile misumari miwili isimamayo mbele ya Mungu wa dunia.

5: Na mtu yeyote akiwapiga, moto unatoka kwa vinywa vyao na kumla, na mtu yeyote akiwaumiza, yeye naye atauliwa vivyo hivyo.

6:Hawa wanao uwezo wa kuzifunga mbingu, ili kusinyeshe wakati wa kutabiri kwao: Pia wako na uwezo juu ya maji, kuyageuza ata yawe damu, na kulipiga dunia na kila aina ya maradhi, kiasi wapendacho.

7: Na hapo watakapomaliza ushuhuda wao, mnyama yule atokaye kuzimu atafanya vita nao, na atawashinda na kuwaua.

8: Na maiti zao zitalala bararani za huo mji mkuu, ambao kiroho unaitwa, sodoma na misri, alikosulubiwa mwokozi wetu.

9: Na watu wa mataifa, kabila lugha na koo wataitazama miili yao kwa siku tatu na nusu, na wala hawatashughulika kuwazika.

10; Na wote wakaao duniani watafurahia kufa kwao, na kusherekea huku wakipatiana zawadi; maana hawa mashahidi wamewafedhehesha wote wakaao juu ya nchi.

11: Baada ya siku tatu na nusu, roho ya uzima ya Mungu ikawaingia, nao wakasimama, na hofu kuu ikawaingia walimwengu wote walipoona wamefufuka.

12: wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, njooni hapa juu, nao wakapaa juu kwa wingu, huku maadui zao wakiwatazama.

Ukifikiria vitendo vya walimwengu dhidi ya mashahidi wa Mungu wakati huu wa miezi arobaini na mbili, kabla ya ujio wa pili, sio ajabu, itachukua malaika wa Mungu mwenye nguvu kuujulisha uma kile kiwango cha udanganyifu wanaoukumbatia. Tunausoma huu utangazo wa malaika, kwenye kurasa tatu baadaye.

Ujumbe wa malaika watatu, Kwa Waliopona katika dhiki kuu

Ufunuo.14:6. Nikaona malaika mwingine akipaa katika mawingu, mwenye injili ya milele, akiwahubiri wao wakaao juu ya nchi, kila taifa, kabila, lugha na ukoo,

7: akisema kwa sauti kuu, ‘ Mcheni Mungu na kumtukuza yeye; kwa maana saa ya hukumu yake imefika: Mwabudini yeye aliye ziumba, mbingu, nchi, bahari na vyote vilivyomo.

8: akafuata malaika mwingine, akisema, ‘ Babeli imeanguka, imeanguka, huo mji mkuu, maana umewafanya mataifa yote kunywa mvinyo wa gadhabu ya uisherati wake.

9: Akafuata mwingine wa tatu akisema, ‘ mtu awayeyote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, , na kupokea alama kwa kipaji cha uso au, mkono wake,

10: huyo atakunywa mvinyo wa gadhabu ya Mungu kwenye kikombe kisiochanganywa; naye atateswa kwa moto na kiberiti, mbele ya malaika watakatifu, na ya mwana kondoo:

11: na moshi wa mateso yao, upaa milele na milele:, na hawana pumziko, mchana wala usiku, hao wasujudio huyo mnyama, na kupokea alama la jina lake.

Huku, mafundisho ya dini za ulimwengu zikiwa zimeimarishwa vile zilivyo,, kama inavyodhihirishwa na kutokuaminiwa kwa mashahidi wa Mungu wakati huu wa mwisho, na kulingana na vile watu wamedanganywa na wahubiri wa kila aina ya Imani, itachukuwa malaika kushinda huku kutokuamini na kujiuzulu kwa waaminio na wasioamini pia. Hata hivyo, kunao wale ambao bado, wataamua kuendelea na Imani zao za udanganyifu, wakionelea ni njema. Hii inaleta hitaji la kukatiliwa na kuangamizwa kwa hizo Imani na matendo yake.

Kuchunguza upya, Mambo Muhimu ya Huu Ujumbe wa Injili

1: Kunao Kusudi Kuu Inayofunuliwa kwa Mwanadamu.

a)Uhai kama tuujuavyo ni kitu cha ajabu katika hii anga letu

wanadamu kila wakati huwa wanashangaa kama kuna sayari nyingine zenye uhai. Wanasayansi wakuu hawajaweza kuthibitisha hilo. Ata jambo la rahisi kama kujua ikiwa kunao sayari yenye mazingira yawezao kuimarisha uhai haijafikika.Lakini sasa, uhai utoka wapi? Hiyo pia ni swali ambalo wanasayansi hawawezi kulijibu.Haifanyiki tu kwa bahati. Hivyo basi, kwa nini kuwe na uhai mahali pengine ikiwa muumba mwenyewe hakuuweka? Ufunuo utokanao na kifungu cha Mwanzo.1, kwamba, mungu aliumba mwanadamu kwa mfano wake ni wazi. Sio kule kuvaa mfano wa Mungu tu kwa huu mwili, lakini tunaweza pia, baada ya kuongoka, kuvaa sura yake na kuonyesha tabia zake za uhaki kwa uwezo wa roho yake iliyo ndani yetu. Hiyo utegemea, ikiwa tutaamua, na kumruhusu aumbe sura yake ndani yatu, kwa uwezo wa hiyo roho yake ikifanya kazi ndani yetu. Hiyo ufanyika tu kwa wale ambao wametubu kwa ukweli, na kubatizwa.

Mwanzo.1:1. Hapo mwanzo, mungu aliumba mbingu na nchi: Ayubu.38:7. Malaika walishangilia kwa furaha dunia ilipoumbwa…kabla ya mwanadamu kuumbwa: Yuda. 6-malaika walipewa kuitawala dunia, lakini wakaacha makao yao: Ayubu.38:4-Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya Dunia?: Mwanzo 1:26-Natuumbe mtu kwa mfano wetu, na kwa sura yetu: Zab.139:14- nimeumbwa kwa ustadi wa ajabu: Wakolosai.1:18,24- Mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu aliviumba vitu vyote: Isaya.40-mataifa yote ni kama tone la maji ndani ya ndoo mbele za Mungu: Isaya.45:18-Mungu aliiumba dunia ikaliwe: Zab.132:14-Mungu mwisho mwisho ataishi duniani hata yeye: 1Wakor.15:24-28-Makao makuu ya anga yote yatakuwa duniani baada ya Mungu baba mwenyewe kushuka:

b) Mungu anaumba jamii iliyo kama yeye

Kwa kuumba mwanadamu aliye kwa mfano wake ni thihirisho kuwa, Mungu anataka kushirikisha wanadamu katika maisha yake ya utukufu. Kwa muda tusiyoweza kujua, Mungu alishiriki maisha yake na malaika wake, huku wao pia wakiwa, waliumbwa, wakiwa na uhuru wa kuchagua.Tunaarifiwa kuwa, theluthi moja yao waliamua kumfuata malaika mkuu aliyeamua kuasi, wakawa pepo wabaya.Malaika waliumbwa wawe mawakala wakufanya kazi wakiunga mkono kazi ya Mungu, wakiangalia na kuimiza mambo kuhusu wale ambao anaita kwa wokovu. Sio kutoka kwa malaika ambapo Mungu anataka kuumba watoto wake.Hao wana, baada ya kufufuliwa wakiwa viumbe wa kiroho, watashiriki maumbile yake wakiwa na kutokuharibika kikamilifu. Maandiko yanaita hiki kitendo, “kuzaliwa mara ya pili”, ambako kunawezeshwa na huyo roho aliyetupa. Kiwango cha huyo roho kinatoshana na Imani ya mtu binafsi.

Mwanzo.2:7- Mungu akaumba mtu wa udongo wa ardhi….mtu akawa kiumbe hai: Mwa.5:1-Mungu akaumba mtu, akamuumba kwa mfano wake: War.8:15-….roho wa kumiliki, ambao kwa huyo, tunalia Abba, baba: waga.4:5- Ili tupokee wenyeji kama wana: Waef.1:5- …aliokusudia kutufanya wana katika Kristo: Waeb.2:10- Mungu anawaleta

wana wengi kwa utukufu…. Taifa lililotukuka baada ya ufufuo: 2petro.1:4-Ahadi za thamani kuu…..tuweze kuwa washirika wa utauwa: War.9:26-Hapo, wataitwa wana wa Mungu aliye hai: War.8:19-uumbaji unaugua ukitazamia kuthihirishwa kwa wana wa Mungu;

c) Kristo atatawala dunia yote kwa muda wa miaka elfu moja

Ijapokuwa dini nyingi asikubaliani na hayo, Kristo akirudi atayatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma.Fimbo ya chuma umaanisha kwamba, hakutakuwa na nafasi ya mtu kuleta mawaitha yake.Hii serikali yake ya haki haitajengwa kupitia upendeleo au kusikizana. Mungu anajua kilicho cha haki. Dini pia zitabadilishwa, zifuate namna ya ibada ambayo ni yeye ataipanga, huku kila namna ya ibada za wanadamu zikikomeshwa kabisa. Huu wakati ndio unaojulikana kama mileniamu, ikimaanisha, kipindi cha miaka elfu moja.

Ufu.2:26- Yeye ashindaye na kuyafanya matendo yangu….nitampa hukumu juu ya mataifa: Ufu.3:21-ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi:Dan.7:27-Tawala zote na mamlaka yatamtumikia: Ufu.2:27- atawatawala mataifa kwa fimbo ya chuma: Isa.2:3-4- Sheria itatoka zayuni: Isa.9:6-Na serikali itakuwa mabegani mwake, naye atatawala miaka elfu moja:

d) wateule wake watatawala pamoja naye kama wafalme na makuhani

Wote wale watakaoshinda, wameahidiwa nyathifa za uongozi katika ufalme wa Mungu hapa duniani. Kunao wale watakaopewa uongozi wa kiutawala, huku wengine wakipewa uongozi wa kikanisa, yaani ukuhani. Yesu mwenyewe atakuwa ndiye mfalme mkuu. Mfalme Daudi wa Israeli atafufuliwa na kuwa kiongozi juu ya nyumba yote ya Israeli(kabila kumi na mbili), huku, mitume kumi na wawili wakipewa kila mmoja kuongoza kabila moja ya hizo kumi na mbili, chini ya mfalme Daudi. Sasa hivi, ulimwengu mzima unaugua, ukitazamia kufanyika kwa wana wa Mungu, baada ya wateule wamefufuliwa wakiwa viumbe wa kiroho, wakati wa panda ya mwisho, na kupewa utawala ili warekebishe maisha na kuyaweka kama vile Mungu alivyoyapanga tangu mwanzoni.

Ufu.5:10- wateule kuwa wafalme na makuhani……wakitawala dunia: Ufu.20:4- wakawa hai na kutawala pamoja na kristo miaka elfu: Dan.7:18- Wateule wa Mungu watapewa ufalme: Dan.7:27- na falme na mamlaka chini ya Mbingu , yatapewa wateule wake aliye juu: Dan.2:44-Ufalme wa Mungu duniani hautaachiwa wengine: Ezek.37:24-25- Daudi, mtumishi wangu atakuwa mfalme juu yao….Israeli…milele: Mat.19:28- Nyinyi kumi na wawili mliofuatana nami, mtakaa kwenye viti kumi na mbili vya enzi:

e) Mteule ni mtu wa aina gani?

Kunao dini Fulani ambayo, imeweka mipango ya kuwachagua baadhi ya wachungaji wao na kuwafanya wateule. Tukifuata maana ya kibiblia ya mteule, utakuta kwamba, kwa hakika, hawa sio wateule. Mteule wa kweli ni mtu aliyeitwa na Mungu, na akaongoka kwa kupokea roho takatifu. Watu wote ambao wameongoka, kwa hii njia ya kupokea roho ya Mungu, ni

wateule.Haihitaji kuamuliwa na mkubwa Fulani wa kanisa, maana hakuna mtu awezaye kuujua moyo wa mwanadamu isipokuwa Mungu pekee. Isitoshe, kabla hiyo dini(katoliki) haijaanza, kulikuwa na wateule wengi.

Ufu.14:12- wateule ni wale wazishikao amri za Mungu na Imani ya Yesu: Yuda.3- wokovu wa jumla….imani iliyopeanwa kwa wateule: 1Wakor.16:1- Kuhusiana na matoleo ya wateule: 1 Wakor.1:2-waliotakaswa ndani ya kristo, ambao ndio wateule:

f)huo ulimwengu ujao ndio ufalme halisi wa Mungu

Ukristo wa siku hizi, hauelewi kimamilifu maana ya ufalme wa Mungu. Kwa wengi, kanisa ndio huo ufalme, yaani, kundi la waaminio. Kanisa wakati huu ni kundi la walioongoka ambao ndio watakaourithi huo ufalme siku za usoni. Lakini ufalme wa Mungu ni utawala utakaoitawala dunia baada ya Kristo kurudi mara ya pili, ambao utakuwa punde tu, dhiki kuu ikiisha. Hapo ndipo Kristo na wateule wataanza kuitawala dunia kwa miaka elfu, wakati ambao, shetani na pepo wabaya wenzake watafungwa. Yerusalemu itaimarisha kama mji mkuu wa dunia yote na amri itakuwa inatoka pale. Wateule watakaa duniani wakitawala pamoja na Kristo juu ya wote wa wanadamu watakaobakia baada ya dhiki kuu, na pia wale watakaozaliwa wakati huo wa miaka elfu.

Ufu.11:15- Falme za dunia hii zimekuwa falme za Bwana wetu: Zekar.6:13- Ataketi… na kutawala juu ya kiti chake cha enzi: 1Wakor.15:24-25- atakapoangamiza mamlaka yote..lazima atawale mpaka…: Ufu.2:27- Atawatawala kwa fimbo ya chumba: 2Petr.3:13- Ahadi yake….dunia mpya ambako uhaki unadumu: 1wakor.15:50- Nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu: Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuurithi ufalme wa Mungu:

g)Sabato ya siku ya saba ni onyesho ya huo mpango

Wiki ya siku saba ilianzishwa wakati wa uumbaji.Aliyeiumba dunia, alipumzika siku hiyo ya saba.Huu mpango wa siku saba za wiki unaachilia mpango wa siku sita-miaka elfu sita, aliyopewa mwanadamu kufanya kazi zake, huku elfu moja ya saba ikiwa ni utawala wa Kristo pamoja na wateue. Hapo Yesu atakaporudi, ulimwengu wote utaanza kuitunza sabato ya siku ya saba(yaani jumamosi).

Mwanzo.2:2-Mungu akamaliza kazi yake…akapumzika siku ya saba: Waeb.4:4- Mungu akapumzika siku ya saba kutoka kwa kazi yake: Waeb.4:9-10- Utunzaji wa sabato bado hupo kwa watu wa Mungu: Waeb.4:1, 10- Kinachoongelelewa hapa ni kuingia kwenye pumziko ya utawala wa miaka elfu moja:2Pet.3:8- siku moja kwa Mungu ni kama miaka elfu moja: Isa.66:23- Kutoka sabato moja adi nyingine, wanadamu wote wataabudu:

h)Sikukuu za biblia pia zinaonyesha huo mpango

Kuendelea kuthibitisha mpango wa ukombozi wa mwanadamu, misimu ya mavuno katika ukulima, inaonyesha, vile Mungu amepanga nyakati ambazo atazipitia kumkomboa mwanadamu.Mungu alitupa seti mbili za sikukuu zake, ili kutufundisha hizo hatua zake za ukombozi, sikijulikana kama, mafuno ya kwanza na ya pili. Ya kwanza inawakilishwa na siku

ya pasaka mpaka pentekosti, ambayo ni kwa wachache wanaoitwa wakati huu. Ya pili, inayowakilishwa na sikukuu ya tarumbeta, mpaka siku ya vibanda, ni wito kwa ulimwengu wote. Ambao walikufa kabla hawajaitwa, hawajapotea maana, sikukuu ya siku ya mwisho, ni wakilisho la wakati ambao, watafufuliwa na kupewa nafasi. Kwa hivyo, hapa tunaona mpango wa Mungu wa ukombozi, katika hatua zake. Haya yanathibitishwa na Yesu katika yohana.6:44; 7:37-38. Hii inathibitisha kuwa, siku ya wokovu sio hii peke yake. Mungu anao hatua kadhaa za wokovu, kulingana na atakavyoita kila mtu.

Yohana.6:44- Hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na baba aliyenituma: Yakubu.5:7- Wakati huu, Mungu anadumisha uvumilivu mkuu, akingojea kutimia kwa hizi nyakati mbili za mavuno: Ufu.22:17- mwenye kiu na aje, atakaye pia aje, anywe maji ya uzima,ona yohana.7:37 pia: Ufu.22:17 ni wataki, baada ya Kristo kuja mara ya pili:Wakolo.2:17- sikukuu za Bwana ni wakilisho za mambo halisi- ni unabii(ukitaka kujua mengi kuhusu hili jambo, soma ujumbe wetu uitwao, " Roho ya sabato za Bwana", upatikanao katika, www.endtimecog.org"): Isa.49:8- hii ndiyo siku ya wokovu(2Wakor.6:2).

i)sikukuu za kawaida za madhehebu usherekea uongo

Huku sikukuu za Bwana sikiwakilisha mpango wa Mungu kwa maisha ya wanadamu, sikukuu za madhehebu ya dunia hasina timizo lolote. Mfano ni kama vile, yesu hakuzaliwa mwezi wa kumi na mbili(soma yeremia.52:31- utaona wababeli wakisherekea hiyo siku,miaka mingi kabla kuzaliwa kwa Yesu), wala hakusulubiwa siku ya ijumaa, au kufufuka jumapili.Sikukuu nyingi wanazosherehekea madhehebu ni za kipagani, huku sikipinduliwa majina tu kufunika uongo wake.

Mat.15:9- Noa wananiabudu bure huku wakifundisha mafundisho ya wanadamu: Jerem.10:2-3- Msienende kama mataifa…maana mila zao ni za bure: Jerem.7:18- Wanatengeneza keki kwa malkia wa mbinguni: Marko.7:8-9- Wananiabudu bure:

2. wote wataitwa na Mungu kwa wakati wake

a)Wachache wameitwa kwa wokovu sasa

Usemi wa Yesu wa wasi kwamba, hakuna awezaye kuja kwake kabla kuvutwa na Mungu, unafurugwa na wengi wa wanaojionyesha kumfuata, wakati wanasema kuwa wakati wa wokovu ni huu peke yake. Hii wanafanya kwa kutokuelewa maana ya kifungu kinachosema kuwa, wakati wa wokovu ni sasa-2 Wakor.6:2. Ukweli ni kwamba, hiki kifungu kinaongea juu ya wale Mungu amewafungua macho kwa kuwaita, na sio kwa kila mtu.

1petr.4:17-Hukumu inaendelea kwa nyumba(kanisa) ya Mungu sasa, sio kwa ulimwengu: Ufu.14:7- baadaye, hukumu inatolewa kwa watu wote: Mat.20:16- Wengi wameitwa, lakini wateule ni wachache: Ufu.17:14- Watakaoitika na kufaulu kuumbika uhaki, hao ndio wateule: War.2:4- Wanaoitwa,uingizwa kwenye toba,….sio kabisa, chaguo lao: yohana.- yeye ndiye ufufuo na uzima……waaminio watapewa hiyo:

b)wengi Hawajaitwa wakati huu

Kama inavyotakiwa kueleweka, Wengi wakati huu hawana nia ya kumtafuta Mungu wa kweli, wala hawana haja ya kutubu. Wale wameitwa peke yao ndio wakati huu, lazima waitikie na kutubu, lakini kwa wengine, ni mpaka hapo wakati wao utakapofika-ona.Luka.10:22. Basi je, wale ambao watakufa kabla yesu kurudi, itakuaje? Siku yao itakuja, lakini hiyo, tutaelezea baadaye.

Matendo.28:27- maana mioyo ya hawa watu imepumbaa…macho yao yamefungika: Mat.13:15- Kristo amewaachilia wengi kwa wito wa baadaye: War.11:8-10- Mungu amewapa roho ya usingizi, macho yasioweza kuona: War.11:7- Wateule wameipata, lakini wengine, wamepofushwa:Marko.4:13-20- Inaeleweka kwamba, sio mbegu zote sinaopandwa zitatoa mbegu za wana wa ufalme:

c)wengine wamepofushwa makusudi

Katika vifungu kama Yohana.6:44; 12:40;War.11:7, tunashuhudiwa vile Mungu amewapofusha wengine makusudi ili wasiweze kuelewa. Vifungu kama hivi utumika na watu wasio na ufahamu, kusema kwamba, kila mtu alipangiwa hata kabla ya kuumbwa; hivyo kumaanisha, kunao wengine watatupwa kwa ziwa la moto bila kuhukumiwa. Lakini, hapa, Mungu ametuonyesha kwamba, wale ambao wamepofushwa kwa sasa, ni kwa muda tu, kwamba, wakati wao kufunguliwa macho utafika.

2 Wakor.4:4- Mungu wa ulimwengu huu amezipofusha akili za wasioamini: Yohana12:40- Mungu amewapofusha, na kufanya mioyo yao kuwa migumu, wasipate kuelewa:Ufu.12:9- Shetani ameudanganya ulimwengu wote: War.11:7- Israeli hawajapata wanachotafuta….; wengi wao wamepofushwa: War.11:32- Mungu amewatia kwa upofu: 2Wakor.3:14-18- Pasia ifunikayo nyuso zao haijaondolewa: Mat.11:25- Baba amechagua wale anataka waelewe wakati huu:

e)kuitwa kunaanzisha uhusiano wa upendo, wa mtu kwa mungu, na kwa wandugu

Jamii ya Mungu ni kundi lililojenga juu ya upendo. Tunaambiwa kwamba, Mungu ni upendo, na kwamba, tunapaswa kuonyesha huo upendo, sio kwa Mungu tu, mbali kati ya sisi wenyewe. Alitupenda ata kabla hatujajua kama yeye yupo, na anataka tuweze kushirikiana naye katika hayo maisha yake milele. Kanisa la Mungu ni kundi la wanaoshirikiana naye kwa njia la roho yake. Kanisa la sasa ni wale wameitwa ili wafundishwe, kusudi waweze kutawala pamoja naye atakapouanzisha ufalme wake.

1Yohana.4:19- tunampenda maana alitupenda kwanza: Waef.2:4- Kwasababu ya upendo mkuu aliotupenda nao: Yohana.13:1- Akiwa amewapenda walio wake ulimwenguni, aliwapenda mpaka mwisho: 1yohana.4:7- Pendaneni nyinyi kwa nyinyi, maana upendo ni wa Mungu: Yohana.14:15- Mkinipenda mtazishika amri zangu: 1 Yohana.3:10-11- Ambaye atendi haki si wa Mungu: 1 Yohana.2:9- asemaye anaenenda katika nuru, huku akimchukia ndugu yake, ubakia gizani: yohana.3:29- aliye na Bwana arusi ndiye bi arusi:

f)Shetani atafungwa wakati wa mavuno ya pili

Tofauti kubwa iliyopo kati ya wakati huu wa miaka elfu sita ya mwanadamu, na wakati wa miaka elfu moja ijayo, ni kuondolewa kwa shetani, na malaika wenzake.Hebu fikiria ufalme huo utakvyokua bila ushawishi wa pepo wabaya, na roho ya uharibifu,ilyo mioyoni mwa watu leo! Shetani atafungwa kwa miaka hiyo elfu moja, lakini baadaye, ataachiliwa. Baada ya kushindwa kwake,na kufa kwa wale, baada ya miaka elfu, watashirikiana naye, ataondolewa kabisa katika uma, na kutupwa kwenye ziwa la moto.

Ufu.20:1-2- Malaika amfunga shetani katika kusimu… kwa miaka elfu moja: Ufu.20:7- Kufungiliwa kwake baada ya miaka elfu, na kujaribu kushambulia kambi ya wateule: Ufu.20:10- Kushindwa kwa mwisho kwa Shetani, kutamuondoa na kukatiza uhusiano wake na wanadamu milele:

3. Amri za Mungu ni Msimamo wa Milele

a)amri za mungu zinaeleza uhaki wa kweli

Mtume paulo anaeleza kwa ufahamu, kuwa, hangeweza kujua dhambi ni nini kama amri haingelieleza. Hizi amri kumi zilikuwako tangu milele, ata kabla kuumbwa chochote kile. Ni ajabu vile, ile sheria moja ambalo ndilo yenye kueleza, umilele, na ambalo limewekwa kama ukumbusho, ndilo dini za dunia hii sinataka kuondoa, yaani- sabato-Kutoka.20:8-11.

Waeb.4:4- Na Mungu akapumzika siku ya saba kutoka kwa kazi yake yote: Mwa.2:2-3- Alipumzika siku ya saba: War.7:12- Amri ni takatifu, ya haki na njema:

b)Dini za kimila upuuza utunzaji wa sheria

Dini za kimila zimepuuza na kuondoa umuhimu wa kutii amri za Mungu katika maisha yao. Badala yake, wanaimiza neema ambayo inaonyesha, utiivu wa sheria kuwa kitu kilichopitwa na wakati. Katika uinjilisti wao, yeyote anayeonekana kufundisha utiivu wa sheria upingwa vikali na ata kutupwa nje la kundi. Kulingana nao, kutii sheria ni kujaribu kupata haki kwa matendo ya sheria.Ijapokuwa ni kweli kwamba, wokovu ni kipawa, na sio malipo ya matendo ya mtu, kunao vile tunapaswa kufanya ndiposa tupewe huo wokovu.

Wakolo.2:14- Sheria haikupigiliwa msalabani; malipo ya dhambi zetu(kifo)yalipigiliwa hapo: War.6:1- Tunatakiwa kuwacha dhambi baada ya kuwa chini ya neema: War.6:15- Tusemeje basi! Tutende dhambi ili neema iongezeke? Mungu anakataza: War.7:22- Paulo kila wakati aling'ang'ania kuishi kwa utiivu wa sheria: War.6:14- Dhambi haipaswi kuwa na hukumu juu yetu kama ilivyokuwa awali: Mat.15:9- sheria zilizowekwa **na wanadamu zimechukuwa nafasi ya sheria za Mungu: Wafilip.2:12- Lazima.. tufuatilie wokovu wetu kwa kicho na kutetemeka:**

c)Yesu hakuondoa sheria wala manabii

Tunaonya dhidi ya kudhania kuwa, Yesu alikuja kutangua torati na manabii. Hata hivyo, Dini za ukristo wa kimila zinafundisha hivyo. Hiyo ni kinyume na maandiko, maana mpango wa agano jipya ni kuziandika sheria za Mungu mioyoni mwa wanadamu, kama inavyoonyeshwa katika agano jipya na la kale pia. Wao udhania kuwa agano la kale ni mambo ya Mungu

baba, na kwamba, Yesu alikuja kulete mapya kwasababu ya kale yamepitwa na wakati. Hiyo fikira inapingwa vikali, tunapogundua kwamba, yule Mungu aliyewaongoza waIsraeli jangwani, akawapa amri kumi huko Sinai, ndiye baadaye alikuja kama Yesu. Ikiwa ni hivyo basi, kwa nini Yesu atupilie mbali kile yeye mwenyewe alipeana? Kwani, ni yeye mwenyewe atunze sabato, halafu aambie watu wasiitunze?

Mat.5:17- Msidhanie kwamba nalikuja kutangua torati au manabii: Waeb.8:10; soma pia Jerem.31:33: 1Yohana.2:4- Ambaye hazishiki **amri za Mungu, hamjui: War.7:25- Paulo anatafuta nguvu za Mungu zimwezeshe kuzishika amri zake:**

d)Alizitimiza sheria kutuonyesha mfano wa vile tunapaswa kuishi

Uongo mwingine wa hizi dini ni kwamba, Kristo alizitimiza sheria, kwa hivyo, sisi hatuna haja ya kuzitunza; yaani, alizitunza kwa niaba yetu. Kutimiza sheria kwa mtu, hakuwafanyi wanaofuata nyayo zake wasitende vivyo hivyo, la sivyo, basi wao hawazifuati nyayo zake. Kuonyesha mfano ni kwa ajili ya, kielelezo kwa watakaotaka kufanya kama yeye.

1Pet.2:21- Kristo alituachia kielelzo ili tufuate nyayo zake(utiivu wa sheria): Ufu.14:4- Wazaliwa wa kwanza ni wale watakaomfuata Yesu kila aendako: 2Tim.2:22- Tafuta uhaki, Imani, upendo na Amani pamoja na wale wamwitao Bwana: Ufu.12:17- Wale wazishikao amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu:

e)Uvunjaji wa sheria ni dhambi

Wakristo wote, wa kweli na wa uongo, uamazisha na kuonya kuhusu dhambi.Tunaambiwa kuwa mshahara wa dhambi ni mauti na kwamba, wote walitenda dhambi. Hiyo inamaanisha kwamba, wote wanafaa kufa. Ile maana ya dhambi, ndio ambayo inaitajika hapa, ili watu wajue, na kuiwacha wasife. Watu wanazo maana nyingi, ambazo zinajaribu kuepa ukweli kwamba, dhambi ni kuvunja amri za Mungu.

War.6:23- mshahara wa dhambi ni mauti; Ezek.18:20;18:4- Yule atendaye dhambi atakufa: War.7:7-sheria sio dhambi. zinaeleza dhambi ni nini: 1yohana.3:4- dhambi ni uvunjaji wa sheria: War.3:23- wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.

f)Neema ufungua njia ya kusamehewa dhambi, sio ruhusa ya kutenda dhambi

Katika kushughulikia kuwacha dhambi, tunaletwa kwenye kazi ya neema.Kwa vile kusamehewa dhambi hakuwezi kuja kwa bidii za matendo yetu, basi inatubidi tujikabidhi kumlilia Mungu atuhurumie. Lakini je, kuna masharti ya kupokea msamaha wa Mungu? Msamaha ndio haswa, ile neema. Neema ni msamaha usio na masharti, sio kwamba tumeuomba au kufanya chochote ndio tupewe, ila, ni mapenzi ya Mungu. Lakini sio vile wengi wandanganyao, kuwa, hatuitaji mabadiliko yoyote katika maisha, bora tu umkubali yesu. Lazima tuwache kile kinachotufanya tuhitaji huo msamaha ambaco ni, kuvunja amri za Mungu(dhambi).

War.6: 1-2- Mungu anakataza watu kuendelea na dhambi wakishasamehewa: War.6:15- Kuwa chini ya neema sio ruhusa ya kuendelea kuvunja amri: 1Yohana.1:8- kutokuwa na dhambi ni hali ambayo inahitajika kuhifadhiwa: War.8:7-8- Roho ya Mungu ndio nguvu zinazotuwezesha kutii amri zake: 1yohana.1:9- Kuungama dhambi ni hitaji la kila wakati, ikiwa tutahifadhi utakaso.

4. Umuhimu wa agano

a)Agano utoa habari kwa mhusika

Maandiko ya Mungu ndiyo ushuhuda wake kwetu sisi wanadamu. Yanaelezea mapenzi yake. Ni ushahidi kwetu,aidha unaotuunga mkono au, unaotupinga kulingana na vile tunaoupokea(yaani, kuukubali ama, kuukataa). Neno la Mungu utushuhudia kuhusu yale maisha ya kweli.

Kumbukumbu.30:19- Mbingu na ardhi zishuhudie dhidi yenu leo…chagueni uzima au mauti: Waeb.12:1- Mmezungukwa na wingu la mashahidi: Waeb.3:16- Wengi, waliposikia, walipuuza, lakini sio wote: War.10:21- Mungu utoa nafasi sizizo za kawaida kwa wale aliowaita.

b)Agano ni makubaliano kati ya wawili

Tukisha fahamishwa umuhimu wa ushuhuda Fulani, tunawekwa kwenye hali ya kuchagua kuukubali au kuukataa.kuukubali kunaachilia mapatano kati yetu na aliyetushuhudia. Hii ndio inaleta maagano kati yetu na Mungu. Ni muhimu sana kufahamu tofauti ya agano na shuhuda. Kwa vile agano la kale na jipya, zote zimejenga juu ya msimamo mmoja wa uhaki, yaani- amri za Mungu, haitupasi kudhania eti sheria zilitupiliwa mbali.

Waef.2:12- Ubatizo uthibitisha kujikabithi kwetu, kwa huu wito na namna ya maisha: Waeb.8:8- Tohara ilikuwa thibitisho la agano lakini haikufaulu: War.2:25-29- Leo, tohara ya moyo ni hali ambayo inafaulu: Kutok.19:5- Uhusiano wa agano utufanya kuwa watu spesheli kwa Mungu: Kutok.31:16- Utunzaji wa sabato ni agano ya milele, kwa vizazi vyote: 2Wafalme.17:38- Na msiwahi kusahau hii agano nimefanya nanyi leo: Nehemia.1:5- Mungu uhifadhi agano na huruma kwao, wazishikao amri zake: Zab.111:9- Aliamrisha agano lake milele:Ezek.2037- Na nitawaleta kwenye kifungo cha agano: War.11:27- Na hii ndiyo agano langu kwao, hapo nitakapowaondolea dhambi: Waeb.8:6- Ni mpatanishi wa agano bora.

c)Ubatizo uthibitisha agano la mtu na Mungu

Mara nyingi, watu utafuta ubatizo bila ufahamu kamili wa yale maisha wanayojiingiza kwayo. Hiki sio kitendo cha kuchukuliwa kwa urahisi. Kwa vile huku kuingizwa kwa haya maji umaanisha kufa na kuzikwa kwa maisha yetu ya awali, tunapaswa kudumu kwenye huu upya wa maisha mpaka mwisho. Ijapokuwa wengi wa wajiitao wakristo usherekea kile wanaita meza ya Bwana kwa nyakati walizozipanga, chanzo cha hiki kitendo kilikuwa wakati Kristo aliketi mezani pamoja na wanafunzi wake muda mfupi kabla ya kusulubiwa kwake. Ukristo aliouanzisha Yesu unaadhimisha hiyo meza ya Bwana(pasaka) mara moja kwa mwaka. Kwa

kuadhimisha hii siku, tunaifanya upya, agano letu na bwana wetu; na ambaye asiyefanya hivyo, anahatarisha kutengwa na Bwana milele- yohana. 13:8.

Matendo.2:38-Tubuni, mkabatizwe kila mmoja..mpokee msamaha wa dhambi: Luka.22:15- Akasema…Nimetamani kuila hii pasaka pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu: Yohana.13:8- Yesu akamwambia..' nisipokuosha miguu, hauna sehemu kati yangu: Yohana.1:12- Wote waliompokea, amewapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu: Marko.1:15- Wakati umewadia, na ufalme wa Mungu ukaribu;Tubuni, mkaiamini injili: Luka 3:3- Wakihubiri ubatizo wa toba kwa msamaha wa dhambi: Matendo.3:19- Tubuni basi, mkaongoke, mpate ondoleo la dhambi: Matendo.26:20- wapate kutubu na kumgeukia Mungu,na kuonyesha matendo yathibitishao toba: Ufu.3:19- Wengi kadiri niwapendao, uwakemea: basi mwe na bidii, mkatubu.

d)Kuacha agano lako na Mungu uleta kifo

Sio watu wengi uelewa uzito uliopo katika kufanya agano na Mungu. Kwa kuifanya, Mungu pia ufanya agano nasi.Kwa kuingia katika hii agano, Mungu ufungua akili na nia zetu kwa amri zake, ambazo, kwa uwezo wa roho yake, zinaandikwa na kuwa ufahamu, na mapenzi ya mioyo yetu-Kumbukumbu.4:6. Kuanzia hapo, zinafaa kuwa ndizo tamaa na nia za mioyo yetu.

Waeb.10:26-29- Kudhuru kipawa cha roho takatifu uleta hukumu ya kifo: Waeb.12

;25- Usimkatae yeye aongeaye nasi: Luka.19:27- Wale ambao hawataki niwe kiongozi wao….wakate mbele yangu: Waebr. 10:26-27- Hakuna toba kwa wale upuuza hiki kipawa baada ya kukipokea.

e)Agano jipya imejengwa juu ya amri za Mungu

masharti yote ya agano jipya yameelezwa vizuri sana katika maagano yote mawili(la kale na jipya). Tunachotakiwa kuelewa ni kwamba, kuletwa kwa agano jipya hakutupilii mbali amri za Mungu. Mtu anapoingia kwenye agano jipya na Mungu, amri zizo hizo ndizo uandikwa katika akili na moyo pia.Hizi amri ndizo huwa namna yetu ya kuishi tukishaa ingia kwenye huo uhusiano wetu na Mungu. Tofauti iliyopo kati ya agano jipya na la kale ni kule kuwepo kwa msingi wa upendo, badala ya ule ulikuwa wa woga, yaani kutii kwa upendo badala ya kutii kwa kuogopa adhabu.

Waebr.8:8-10- nitaziandika sheria zangu mioyoni mwao na kuzitia katika akili zao; jerem.31:33: Mat.22:40- Amri kumi ndizo muundo msingi wa torati na manabii;War.7:16- Na kubaliana na sheria ya kuwa ni njema: War.7:12- Amri ni takataktifu, ni ya haki na njema.

f)Agano la kale lilifundisha maadili ya haki kwa taifa lisiloongoka

Tunaweza kushangaa ni kwa nini agano la kale haikuimarika. Kuelewa sababu yake, kunahitaji kuelewa hali ya wale walioipewa. Wao kama taifa hawakuwa wamepewa roho takatifu. Kule kupewa shuhuda na amri hakukutosha kuleta ukamilivu. Ijapokuwa walionekana kukubaliana na Mungu pale Sinai, mioyo yao haikuwa na mvuto

wakuwawezesha kuishika agano. Ijapokuwa kulikuwa na Baraka za kimwili kwa wale walioishikilia kiasi, hiyo haikuleta kuongoka kamili. Wao walibaki kuwa wa kimwili kama wanadamu wengine.Mungu anao mpango kwao wa wakati ujao, ambapo atawaita na kufanya hili agano nao, katika masingira yanayofaa. Na hiyo itakuwa wakati wa utawala wa miaka elfu, hapo yesu atakapokuwa akitawala na wateule.

War.11:26- Israeli wote wataokolewa: Wagal.3:19- Hii sheria iliongezewa kwa sababu ya dhambi: Ufu.20:12- Vitabu vitasomwa kwao ili waelewe: Ufu. 11:19- Hekalu litafunguliwa kwa wote(zamani ilikuwa kwa kuhani mkuu peke yake): Ezek.37:12-14- Katika ufufuo wa pili, Israeli watapewa roho ya Mungu.

5. Kuongoka kwa kweli hakueleweki kikamilivu

a)kwa nini watu wote wanahitaji wokovu?

Kama tulivyoelezea hapo awali, Sisi zote, kwa kule kujifunza kutoka kwa baba yetu Adamu, tulitenda dhami, hivyo kushindwa kumtii Mungu. Katika huu mwili, tumeumbwa na hali isiyoweza kutii amri zake(ujumbe wetu uitwao, " Kususdi la mwili", upatikanao katika www.endtimecog.org, unao maelezo Zaidi).Hakuna mwanadamu uzaliwa akiwa mwenye haki, ambaye hastahili adhabu ya kifo. Sisi zote, baada ya kujifunza kwa wazazi wetu, tumekosa kuumbika tabia za uhaki za muumba wetu.

Yohnan.1: 8- Yohana hakuwa hiyo nuru, mbali aliishuhudia: Zab.14:3- Hakuna atendaye wema ata mmoja: Zab.53:3- wote wamepotoka: War.8:Akili ya kimwili ni uadui dhidi ya amri za Mungu: War.3:10- Hakuna mwenye haki ata mmoja: Isa.55:8- Mafikira na njia zangu sio zile zako.

b)Wokovu na msamaha ni kipawa

Kitu kimoja ambacho kimeeleweka vizuri kwa karibu dini zote ni kwamba wito wetu kwa toba na msamaha wa dhambi ni kipawa cha Mungu. Tunaongozwa kwa toba.Hata hivyo, ni hiyo sehemu ya kipawa imeleta kutokueleweka, maana, hata kama ni kipawa, haijaondoa ile amri ya kumfuata Mungu, kwa kutii amri zake, huku tukipigania kutoa utu wa zamani- Waef.4:22, ambao saa yote uko macho, tayari kuamka mtu anapolegea.

War.2:4- Wema wa Mungu unakuongoza kwa toba: Yohana.15:16- Tunaitwa kulingana na mpango wa Mungu, sio wetu: War.5:18- Ni sadaka Ya Yesu pekee iwezeshayo msamaha, na kuhesabiwa haki: Yohana.1:29- Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu: Isa.53:6- Naye Bwana amemwekelea makosa yetu yote: Tukihesabiwa haki bure,kwa nehema yake.

c)Kuongoka ni kitendo kinachoendelea, maisha yote ya mtu.

Katika ujumbe wa malaika kwa makanisa saba ulioko Ufunuo.2,3, tunaona kwamba kushinda kunahitajika ikiwa tutafikia tulichoahidiwa. Hizo ahadi ni pamoja na, kuuendea mti wa uzima, kupewa jina jipya,,uwezo juu ya mataifa, nguo nyeupe, kuwa nguzo katika hekalu la Mungu, eee, kuketi pamoja na Bwana wetu katika kiti chake cha enzi. Tunatenda dhambi,

maana sisi ni wenye dhambi. Nasema kwamba, ijapokuwa tumesamehewa, bado tuna vita na mwili ambao mara kwa mara, unatushinda na kutuingiza kwa dhambi. Lakini lazima mwisho mwisho tuushinde kabisa.

1Wakor.9:24- shindana ili uweze kuipokea thawabu: Wag.6:9- Tusichoke kutenda wema…..maana mwishowe tutatuzwa:1Wakor.9:27- nauthibiti mwili wangu na kuufanya mateka kumtii kristo: Wag.6:9-Tutatuzwa ikiwa hatutajiuzulu.

d)Tutatuzwa kulingana na matendo yetu

Hili ni eneo lingine ambalo dini nyingi hazilielewi. Katika hiyo Imani yao kwamba, Yesu amemaliza yote, kwa hivyo hatuhitajiki kutenda lolote, isipokuwa kuamini tu, watu wamekana maisha ya Mungu bila kujua. Neno liko wazi kwamba, wateule watatuzwa kulingana na matendo yao. Wenye kutenda madogo, watatuzwa kidogo, makubwa, kikubwa; hata wengine watapoteza kile kidogo wako nacho. Kunao kile kipawa, kisichotegemea matendo. Lakini kunao sehemu nyingine inategemea matendo.

Ufu.2:23- Nitawatuza kila mmoja kulingana na matendo yake: Ufu.22:12- Naja upesi, na ujira wangu mkononi… kuwapa kila mmoja kulingna na kazi yake: 1Wakor.3:14-15- kazi ya mtu…iliyojengwa juu ya msingi…. Itapata zawadi: Mat.25:14-30- Fumbo la talenti inaonyesha tuzo kulingana na kazi ya mtu: Luka.6:35- Kupenda, kuwa mwenye upendo kwa adui kunao tuzo.

e)Imani, toba, ubatizo, zinahitajika kabla ya kupokea roho takatifu

Wengi wa wanaopokea hii injili na kuikubali, mwanzo mwanzo ,udhania kwamba, ni kwa bidii, na kutaka kwao wenyewe. Tunapoendelea kukua, tunakuja kuelewa kwamba, kipawa cha Mungu kwetu uanza kitambo hata kabla hatujaanza kufahamu. Tunaitwa na baba, na kupewa kutubu, na pia kupewa akili ya kuanza kuelewa kile ambacho kimefichwa kwa wengi.Nafasi ya Ile Imani yetu ya kwanza, baadaye uchukuliwa na Imani ya Yesu ndani yetu. Ni lazima basi, tujikabidhi kwa kifo cha utu wetu wa zamani katika ile ishara ya ubatizo, na kupokea roho takatifu kwa kuwekelewa mikono, kupitia kwa mtumishi wa Bwana aliye mwaminifu.

Matendo.2:38- Tubuni, mkabatizwe kila mmoja, mkapokee roho takatifu: 2Wakor.7:10-11- inaeleza aina saba za hali ya toba ya kweli: Mat.3:13- Ubatizo unahitajika kutimiza haki yote: Matendo.2:38- Kupokea roho takatifu kunafuata baada ya ubatizo: Luka.7:29- Ubatizo peke yake ni hatua moja tu…lazima kupokea roho kufuate: Matendo. 8:16-17- Kuwekelewa mikono, ni hitaji katika kupokea roho: 2Tim.1:6- Tumia kipawa kilichoko ndani yako ulichopata kwa kuwekelewa mikono: Matendo. 19:4-6- Walikuwa hawajajua bado mambo ya kuwekelewa mikono.

f)Bila roho takatifu, mtu hajiwezi

Umuhimu wa hatua hii katika kuongoka hauwezi kuachwa bila kuelezewa. Ili tuweze kuwa na ile sura ya Kristo ndani yetu, ni lazima kwanza, kwa kiwango kidogo cha kuanzia, tupokee ule uhai wake(roho) mioyoni mwetu.Ni huo uhai, ambao wengi uita, kuzaliwa mara ya pili,

ambao, lazima ukwezwe. Ni hizo nguvu za roho ambazo uwezesha mtu kuumbika utakatifu. Kuumbika utakatifu hakuwezekani kwa nguvu za mtu binafsi. Kunao viwango katika uwezo wa mtu, ambavyo ufika mahali, vikashindwa kushindana. Bila hiyo roho yake ndani yetu, hatukubaliki kuwa wana wa Mungu. Ni kule kutoshikilia hiyo roho ndani yetu, kwa kuendelea kutenda dhambi kiasi cha kiuwa hiyo roho, ambako kunaleta ile dhambi ya kukufuru. Hakuna ambaye, upuuza hicho kipawa kufikia kukiua ambaye ana nafasi kukipokea tena.

Waebr.6:1-2- Inaelezea, pointi saba, za mafundisho ya kimsingi katika kanisa la Mungu: Yohana.3:3- isipokuwa mtu azaliwe mara ya pili, hawezi kuuona, au kuuingia ufalme wa Mungu: Yohana.3:6-8- Lazima tuzaliwe kwa roho-tufufuliwe/tubadilishwe, na kuwa viumbe wa kiroho: War.8:9- Ikiwa mtu hana roho wa Kristo, huyo si wake: War.8:14- ni wale tu wenye roho ya Mungu, ambao ni watoto wake: Wagal.5:22-25- Walio na roho ya kristo uthibitika kwa hizi tabia(soma).

6. Kutakuwa na ufufuo wa wote ambao wamewahi kuishi

a)wateule wote watafufuliwa wakiwa roho, wakati wa ujio wa pili

Ijapokuwa wengi wa Dini siku hizi wanafundisha mambo ya kuenda mbinguni baada ya kufa, ukweli ni kwamba, watu watafufuliwa siku ya mwisho na kupewa miili ya kiroho.

Ufu. 2:11- yeye ashindaye hataumizwa na mauti ya pili; Ufu.20:6: Yohana.5:24- Waaminio tayari wameepushwa na mauti ya pili: 1 Wakor.15:51-54- wateule wote watabadilishwa na kuwa roho wakati wa ujio wa pili: 1 Wakor.15:20-23- Ufufuo wa wateule wote utakuwa kama ule wa Kristo: 1 Wathes.4:13-17- Wafu watafufuliwa na kutokuharibika wakati wa panda ya mwisho.

b)Kutakuwa na sherehe ya kutuzwa Yesu atakaporudi

Ijapokuwa ni lazima wakati fulani, tusimame mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ukweli wa hukumu wa uzima unaonyesha, tukio lingine, tofauti ni lile la uamusi wa mwisho baada ya hukumu. Washindao watatuzwa kulingana na kazi zao, walizozifanya kwa nguvu za roho takatifu na kuuendea ukamilivu.

Mat.16:27- Kristo mwenye utukufu atawatuza kulingana na kazi zao; 1 Wakor.3:8: 2Tim.4:8- Taji la uzima latungoja, hapo atakapokuja: Ufu.11:18- Wakati wa kutuzwa watangazwa, hapo ajapo Kristo: Ufu .20:5- Watakaofufuliwa, wafurahia maisha kwa miaka elfu moja.

c)Wengi watafufuliwa baada ya miaka elfu moja

Kristo anasema wasiwasi kuwa(waliobakia baada ya ufufuo wakwanza) wengi watabakia makaburini mpaka miaka elfu iishe. Tunaelezwa kwamba kutakuwa na ufufuo wa pili uliotofauti na ule wa kwanza. Lakini ni jambo la kuchunguzwa, kwamba, ni wale tu watakaosikia sauti ikiita kuwafufua, ambao watafukuka, kuonyesha bado kunao ufufuo mwingine baadaye, ambao, wote watasikia. Wengine ufikiria hii kuwa ufufuo wa pili na wa

tatu.Tunaweza kusema ni hatua ya kwanza, na ya pili ya ufufuo katika mwili wa nyama baada ya miaka elfu moja. Yesu anazungumzia kuhusu watu katika nyakati zote, ambao watafufuka na kutambua kutofaulu kwao.

Ufu.20:5- wafu waliobaki wafufuka baada ya miaka elfu moja: Ezek.37:- uonyesha kufufuka kwa wa-Israeli wa kimwili baada ya miaka elfu: 1 Wakor.15:22-23- Kila moja afufuliwa kwa wakati wake: Mat.12:41-42- Waliokufa nyakati tofauti watafufuka na kuchanganyikana; Luka.11:31-32: Yohana.5:25- watakaoisikia hiyo sauti(ufufuo wa kwanza) wataamka, wasione hukumu.

d)Bado kunao nafasi ya wasioitwa wakati huu

Kile hakieleweki kwa wengi ni kusudi la huu ufufuo wa baada ya miaka elfu. Inafikirika kuwa la kuamulia waliohukumiwa tayari, lakini sivyo. Ni nafasi ya hukumu kwa wale wamewahi kuishi na kufa kabla ya kupata nafasi ya kuitwa kwa wokovu. Ambao walipata hio nafasi katika maisha yao, na wakaipoteza, kisha wakafa, watabakia makaburini mpaka uamusi wa mwisho kabisa.

Ufu.20:12- Vitabu vyafunguliwa kuwafahamisha wasioelewa hapo awali: Ufu.20:12-Kitabu cha uzima chafunguliwa pia, kuongezea majina ndani yake: Ufu.7:9-Umati mkubwa waitikia baada ya ule wa mavuno ya kwanza: Ufu.7:13-15- Hawa pia ni wa jamii ya Mungu, na wataishi naye: Isa.65:20- Mwana wa Mungu katika milenia atakufa na kungoja uamusi kama vile sasa: Mat.25:31-46- Wote, wenye haki, kwa wasio haki watafufuliwa kwa uamusi wa mwisho: Ufu.14:14- tamasha la wingu jeupe inaonyesha mavuno ya watakaoongoka baada ya ujio wa pili.

e)Watakaokataa wokovu watajipatia mauti ya pili

Kukataa wito wa Mungu kunao madhara makubwa. Kuitwa na Mungu ni nafasi ya muhimu sana. Kukataa au kupuuza huu wito kunawacha mtu bila nafasi ya kutubu tena. Hakuna atakayehesabia mauti ya pili kabla ya kupewa nafasi ya kuongoka kwanza. Inaweza kuwa hukumu isio ya haki ikiwa, mtu ataamuliwa kufa kabla ya kupewa nafasi ya uzima. Na vivyo hivyo, haitakuwa hukumu ya haki kwa mtu kupewa uzima kabla ya yeye kuamua, na kupitia mafunzo yake(yaani, kushinda). Kupokea baadhi ya haya mawili kutategemea uamusi wa mtu binafsi wa kukubali au kukataa, baada ya kuitwa.

Waeb.6:4-6- Haiwezekani kuleta tena kwa toba, mtu ambaye ameikataa: Waeb.10:26-29-Kukufuru roho takatifu uleta uamusi wa mauti kwa mwenye kufanya hivyo: Mat.25:33, 41-46- Hao wapokea kuangamia kabisa kwenye ziwa la moto: Waeb.10:31- Ni jambo la kuaminika ambapo, wasio haki waondolewa kwa jamii ya Mungu: Ufu.21:8- Wasioamini wataangamia kwenye ziwa la moto ambalo ndio mauti ya pili: Mat.10:28- Mwogope yeye awezaye kuharibu, na kutupa kwenye jehanamu.

7. Kifo cha mwili ni kama usingizi wa muda

a)Kifo cha mwili sio cha milele

Hili jambo linaleta swali kwa hao wanaoamini kwamba watu wakifa uenda aitha mbinguni au kwenye ziwa la moto. Fundisho la kimsingi la biblia linaonyesha wazi kwamba, kunao ufufuo wa wafu kwa nyakati tofauti, wakati ujao. Ufufuo wa wateule utakua ni wa kufanyika viumbe wa kiroho. Wa wale wengine utakuwa ni wa kufufuka kwa huu mwili wa nyama.

1 Wakor.15:40-44- Tutapokea miili ya kiroho katika ufufuo wa kwanza: 1wakor.15:49- Tutavaa umbo la yeye aliye wa juu: 1Wakor.15:52-54- Tutabadilishwa tuwe na kutokuharibika: 1wathes.4:15- Waliokufa katika Kristo watafufuliwa wakati wa tarumbeta la mwisho.

b)mwili sio wa milele

Kulingana na mafundisho ya mbinguni au jehanamu baada ya kifo, huu mwili unaaminika kuwa, usiokufa. Na hii utokana na kutokuelewa, mwili ni nini. Nafsi kwa kibiblia, ni ule uhai wa mtu, sawasawa na wa mnyama. Kunao tofauti kati ya hii nafsi, na roho ya mtu, ambayo umwezesha mtu kuwa na akili ya kupokea ufahamu na kukumbuka, tofauti na mnyama. Ni hii roho ya mtu ambayo, wakati wa kufa, urudi kwa Mungu aliyeipeana. Hii roho sio mtu mwingine ndani ya mwili, mbali ni kitu ndani ya akili ambacho kinahifadhi matendo na fikira za mtu. Hiki ndicho wakati wa ufufuo, kitatumika kuamua yale maisha mtu aliishi.

Ezek.18:4,20- Nafsi ile itendayo dhambi itakufa: Mhub.3:19- Kama vile mnyama hufa, na mwanadmu hufa vivyo hivyo. Wote hufa sawa: 1 Tim.6:16- Mungu peke yake ndiye hafi: 1 Wakor.15:53- Lakini kwa wafauluo, atawapa kutokufa.

c)Hakuna fahamu baada ya kufa

Maandiko yanaonyesha wazi kuwa, baada ya kufo, hamna ufahamu wowote. Hata hivyo, dini nyingi upinga huu ukweli.

Zab.146:4- Mtu akifa, siku yiyo hiyo, fahamu zake upotea: Zab.6:5- Katika kifo, hakuna kumbukumbu lako; nani awezaye kukusifu katika kifo: Mhub.9:10- Hakuna kazi, hakuna ufahamu, hakuna hekima, huko uendako kaburini: 1Wathes.4:14- Hata wale waliokufa katika Kristo, wamelala wakingoja kuamshwa.

d) mauti ya pili ndio mwisho wa waovu

Mtu akihesabiwa kushiriki mauti ya pili bila kupewa nafasi ya wito, atakuwa amedhulumiwa, kitu ambacho Mungu asiye na upendeleo hawezi fanya.Kuelewa mpango wa Mungu kunatatua maswali mengi kuhusu wale waliokufa kabla ya kupata huu wito wa wokovu.

Ufu.20:14- Mauti na kuzimu zitaangamizwa baada ya uamuzi wa mwisho: Ufu.21:8- Ziwa la moto ndio mauti ya pili; waovu wote waangamizwa hapa: Ufu.14:18- Malaika mwenye uwezo juu ya moto, anavuna waovu, kuwaangamiza: Yohana.5:28-29- Ufufuo wa mwisho ni wakati wa uamuzi wa mwisho: mauti ya pili.

e)Kutimizwa katika ziwa la moto

Jambo lingine lisiloeleweka ni kuhusu mwisho wa wale watakaothibitika kuwa waovu. Kinyume na mafundisho ya dini, kwamba watachomwa katika jehanamu milele bila kufa, biblia inasema wazi kwamba, watateketezwa na kuwa majivu, wasiwepo wala kuwa na ufahamu tena.

Ufu.20:14- Ziwa la moto lawateketeza wote waingizwao humo: Ufu.21:8- Waovu wote waangamia hapa: Mat.10:28- Kristo anawaonya wasioamini kuhusu hii siku na hapa mahali(ziwa lamoto).

8. Hukumu ya walio wengi ni baada ya milenia(miaka elfu)

a)Ni wale tu ambao wameitwa na mungu ambao wanahukumiwa sasa

Ni muhimu kuelewa kwamba, ni lazima mtu aitwe na Mungu ndio ahukumiwe. Hii inahitaji kuielewa maana ya hukumu. Hukumu uhuzisha kusomewa makosa, halafu baada ya kuyakiri, kutolewa uamuzi. Hii hukumu sasa hivi ndio inaendelea kwa Kanisa la Mungu(walioitwa pekee). Ni viizuri kuelewa wakati wa wokovu ni huu peke yake, lakini kwa yule ambaye ameitwa, ambaye peke yake, ndiye anayepewa kuisikia na kuielewa hii sauti.

1Pet.4:17- Hukumu inaendelea ndani ya kanisa sasa: Waeb.4:7- Lazima tusikilize na kuitika tunapopewa kuisikia na kuielewa hii sauti: Ufu.20:12- Vitabu sasa hivi vinafunguliwa kwa kanisa peke yake-Mat.13: 10-11.

b)Wengine watahukumiwa baada ya Yesu kurudi mara ya pili

Ni tu, baada ya wateule kufufuliwa na ufalme wa Mungu kuimarishwa, ambapo, watu wote watahukumiwa kwa kufunguliwa kwa vitabu vya biblia. Hapa ndipo ile pasia iwapumbazayo itaondolewa.Malaika watatambulisha dini ya kweli kwa wale wamepitia kwa ile dhiki kuu kwanza, Nao watawafundisha wazao wao. Wote, " watamjua Bwana". Wakati huo huo, dini zote za uongo zitakomeshwa kwa uwezo mkuu na adhabu kali kwa wagaidio.

Waeb.8:12- Wote watanifahamu, toka mdogo adi mkubwa: Ufu.14:6- Malaika atangaza injili ya milele kwa wote walio hai wakati huu: Ufu.11:19- Hekalu na sanduku la angano zitafunguliwa wakati huu: Ufu.20:12- Vitabu(biblia) vitafunguliwa kwa ufahamu wa wote wakati huu: 2 Wakor.3:16- ile pazia uwafunikayo akili itaondolewa wakati huu: Ufu.14:9-11- Ibada za kila aina za yule mnyama zitakuwa marufuku kabisa.

c)Hukumu ya haki ni lazima ianze na kufunuliwa kwa makosa

Haitakuwa haki kwa Mungu kuwahesabia watu kifo kabla ya kuwapa nafasi ya wokovu. Watu wengi ufikiria uamusi kila wasikiapo neno, "hukumu". Kama kwa kila koti, ni lazima makosa yasomwe kwanza, ushahidi upatikane kabla ya uamusi kutolewa. Ni baada ya hapo, hukumu ya haki inaweza kutolewa. Kitambulisho cha aina hii hakiwezekani kwa mtu tu, kusikia wito katika madhabahu, kuambiwa aokoke, halafu iwe tosha kwa uamusi kwamba amekataa au kukubali. Kupewa uzima wa milele na kuingizwa katika jamii ya Mungu

kunahitaji maisha ya kushinda muda wote aishiyo mtu. Lazima pia tujenge na kuthibitisha tabia za wito wetu.

Ufu.14:6- Injili ya milele yahubiriwa na malaika kwa wote walio hai baada ya dhiki kuu: Ufu.14:13- Washindao katika milenia watangojea zawadi zao kama tunavyofanya sasa: Ufu.14:7- Hukumu ya uamusi hapa imetolewa kwa watu wote: Ufu.20:11-Hii inaitwa, "hukumu ya kiti kikuu cheupe cha enzi": 1 Wakor.3:12-14- kuumbika tabia kunachangia kupata zawadi baada ya kupewa uzima wa milele.

d)hukumu hii italeta uamusi wa mwisho

Ni wakati tu, baada ya ushahidi wote umekusanywa, ambapo uamusi unaweza kutolewa. Hakuna mahali popote ambapo, watu ambao hawajaitwa, hawajahubiriwa, wanaweza kwa hakika kuamuliwa kesi. Ni mpaka hali yao iweze kuonyeshwa kwanza.

Ufu.14:14-20- Inaelezea, uamusi katika wingu jeupe: Wengine kwa uzima/wengine kwa mauti: ufu.14:17-20- Inaonyesha mwisho wa wale watakataa kabisa: ufu.21:8- watatupwa kwenye ziwa la moto: Yohana.5:29-Wenye haki kwa waovu wote watafufuliwa wakati wa mwisho kwa uamusi: Mat.25:31-46- Mbuzi, na kondoo hapa, zinaonyesha wakati huo huo.

e)uamusi wa milele-mauti ya pili- ni ya mwisho na ya haki

Ni wakati tu, kila mtu amejichagulia kuwa kondoo au mbuzi, ambapo, mwisho wake unaweza kuamuliwa. Adhabu ya kifo cha milele itakuwa ya haki kwa watu ambao wanao ufahamu wake kamili. Mauti ya pili haihuzishi kuishi milele katika ziwa la moto, lakini ni kufa kabisa.

Mat.25:46- Mbuzi(wale wagaidio) watahadhibiwa milele: Zab.146- Mauti ya pili haihuzishi ufahamu kama vile ya kwanza pia: Waeb.10:27- Mwisho wakuogofya unawangojea wale wakataao kipawa cha roho takatifu: Ufu.21:8- Inaangazia aina ya wale watakaoshiriki mauti ya pili.

Na wanafunzi wake wakaja, wakamwambia, ' kwa nini unaongea na wao kwa fumbo na mithali? Akajibu na kuwaambia, hii siri ya ufalme imepeanwa kwenu kujua, lakini wao hawajapewa kujua. Maana aliye nayo, yeye atapewa, na atakuwa nayo kwa wingi:Lakini kwake yeye ambaye hana, hata ile kidogo alienayo itachukuliwa. Kwa sababu hii, naongea nao kwa mithali: sababu kuona, wasione, na kusikia, wasisikie; hata wasielewe. Kwa hao, unabii wa Isaya unatimia, ule usemao, Kwa kusikia mtasikia lakini hamtaelewa; kuona mtaona lakini hamtashika: Maana mioyo ya hao watu imetiwa giza, na masikio yao yamezibwa, na macho yamepofuka; wasiwe wakaona, na kusiskia, na kuelewa kwa akili zao, na kugeuka nikawaponyesha. Lakini heri macho yenu nyinyi muonao, na msikiao. Maana amini nawaambieni, manabii wengi, na wenye haki walitamani kuona yale mnaoyaona wasione; na kusikia, wala hawakusikia-Mat.13:10-17".

----------MASWALI NA MAJIBU----------

Swali kutoka kwa mchungaji, Afrika mashariki,

Hapa kunao maswali nilipata kutoka kwa viongozi wa makundi, na nayawakilisha kama yafuatayo; majibu yameandikwa kwa herufi nzito Zaidi: Haya maswali yanaonyesha Imani za ukristo wa siku hizi. Kwa maelekezo ya utangulizi, ni muhimu tuelewe usawa au ukosevu wa misimamo Fulani.

1)Yule aliyewaongoza Israeli Jangwani. Paulo anasema kwamba, huyo alikuwa Kristo-1Wakor.10:4; sio Mungu baba. Kunao baadhi ya wa-injilisti wanaofundisha kuwa, aliyepeana amri pale Sinai ni Mungu baba, lakini baadaye Kristo akaja na kuzitupilia mbali maana zilikuwa jeuri kwa wanadamu(kutokufahamu huku). Si kweli, maanake, aliyepeana hizi amri, ni yule Mungu ambaye baadaye alikuja kuitwa Kristo. Kwa hivyo, hizi amri zilipeanwa na kristo mwenyewe. Aliyepeana amri pale mlima Sinai ndiye yuyo huyo ambaye aliwaongoza

2) Fundisho lingine ni kwamba hizi amri na agano ni kitu kimoja. Lakini sivyo! Wanasema kuwa, kwasababu agano lilipita, na vivyo hivyo, amri zilipita. Si kweli. Hii amri ni ile namna ya kuishi ambayo inaitwa uhaki, na ni maisha ya Mungu, ambayo ndiyo maisha yetu. Hakuna kitu kiovu, kizito, au, ambacho hakifai katika amri za Mungu. Sheria ni sheria, iwe mtu ataitunza au la.Agano ni makubaliano kati ya wawili. Agano linaweza kuja na kuenda, ikitegemea kama wenye kukubaliana wataihifadhi(kuidumisha) au la. Sheria haiondolewi, eti kwasababu, mmoja kati ya wakubalianao ameyavunja makubaliano. Hili ni fundisho lililoletwa na kundi mmoja, na kupelekea wengi kuingia katika upotovu mkubwa. Hii amri ni ule msingi wa agano kati ya Israeli wa kale na Mungu. Amri ya Mungu inadumu hata kama mtu ataitii au la. Kama nikikubali kutii amri ya Mungu sasa, halafu baadaye nikatae, kukataa kwangu hakutaiondoa amri, mbali kutaondoa makubaliano(agano). Kwa upande wa amri za Mungu, zinatufundisha vile tunapaswa kumpenda Mungu, na kupendana sisi kwa sisi.

Dhambi ni kuvunja sheria, iwe mtu ako chini ya agano au la. Hatupati uwezo wa kutenda dhambi kwa kufanya agano(makubaliano). Tunafanya dhambi kwa kuvunja amri za Mungu, ambayo haitegemei mtu kuwa chini la agano au la. (kutofahamu nambari 2). Kumbuka, dhambi haikuanzia pale Sinai. Adamu, Awa, Kaini, hawa wote walitenda dhambi, huko kitambo sana kabla kupeanwa sheria pale siani. (war.5:14) Dhambi ambayo ni kuvunja amri za Mungu(1yohana.3:4), Haikuja kwa mwanadamu baada ya kupewa amri kumi, na wala,kuvunja agano kwa Israeli hakukutangua hizo amri. Sheria ya Mungu ni msimamo wa milele.

3) Hizi dini,zinafundishwa kwamba, hii sheria ya Mungu ni jeuri na nzito, na kwamba, Yesu aliibadilisha na kuleta upendo badala yake; kwamba amri zake ni tofauti na zile za baba yake. Sivyo ata kidogo, maana amri hizi ndizo maelezo ya upendo. Ni vile tu, Wayahudi wa wakati wa Yesu walikuwa wameleta mila zao kwa kutafsiri vibaya, maana ya hizo amri. Upendo umejengwa juu ya sheria tangu milele lakini haikuwa ndani ya watu(kutofahamu nambari 3- soma, 1Yohana.2:3-7 na, 5:3).

4) Kutokuelewa kule kukubwa Zaidi ni watu kutotofautisha kati ya kutii sheria, na kuhesabiwa haki. Katika kila mahali ambapo Paulo anaongea kama ambaye anapinga sheria, Inakuwa ni katika hali ya, kuhesabiwa haki.Paulo anaunga mkono sheria isipokuwa tu, wakati watu wanachukulia ni kama, wanaweza kupata wokovu wao wenyewe kwa kutii sheria. Kile anachoeleza ni kwamba, hakuna utunzaji wa sheria uwezao kulipia mtu dhambi alizozitenda hapo awali. Hatuwezi fanya chochote kwa matendo mema au utunzaji wa sheria, kupata ondoleo la dhambi.Dhambi inaachilia hukumu ya kifo. (War.6:23) Lazima umwagikaji wa damu uwepo,ili dhambi iondolewe. Ile fikira ya kwamba, matamshi ya Paulo yanaachilia kufanya amri za Mungu zikose maana ni kutokuelewa. Hii ni Imani inayoshikiliwa na ukristo wa mila(kutofahamu nambari.4).

5) Kuongezea katika huku kuchanganyikiwa, ni hii hali ya watu kutotofautisha kati ya amri kumi zielezao uzima, na amri za huduma, zilizoongezewa na Musa kwa ajili ya

utunzi wa hekalu na mambo ya utoaji sadaka(ambazo ziliongezewa kwa sababu ya dhambi-wag.3:19). Huku akiona vile watu hawawezi kutunza ile agano kwasababu ya umwili, Mungu aliongezea hizi sheria ili ziwe ukumbusho wa kila wakati wa dhambi zao, na pia kuwafundisha vile wanaitaji kupata ondoleo la hizo dhambi. Matendo yao katika bidii ya kuzitii hizi sheria hayawezi kuondoa hizi dhambi. Amri ikishaa vunjwa, lazima damu imwagwe, yaani ,kifo kitokee ili kulipia hiyo dhambi-(Waeb.9:22). Ikiwa hatutakubali damu ya yesu kulipia dhambi zetu, basi itabidi tuzilipie sisi wenyewe kwa kifo katika ziwa la moto. Ijapokuwa, hizi sheria zilizoongezewa zimesitishwa kwa sasa, amri ya uzima(amri kumi), zinaendelea kwa kila mtu (kutofahamu nambari 5).

Sasa turudi kwa haya maswali ya huyu mchungaji

1.Sizitizo la Paulo ilikuwa juu ya, kuhesabiwa haki, " kwa Imani pasipo matendo ya sheria-War.3:28", "Kwasababu, kwa kutenda sheria, hakuna atakayehesabiwa haki-Gal.2:16". Ya nini sasa basi, mkristo ahitajike kushika amri za agano la kale? Kwani, uongozi wa roho takatifu hautoshi? JIBU: **Matamshi ya Paulo ni sawa kabisa.Hatuwezi pata ondoleo la dhambi kwa kuzishika amri. Nambari nne hapo juu limeelezea hili jambo. Watu siku hizi wanakosea wanapoanza kufikiria eti kunao njia tofauti ya kuishi bila kutii amri ambazo ndizo maelezo ya maisha. Anachoweka wasi hapa ni kwamba, utunzi wa sheria, na matendo ya haki, hayawezi kufanya dhambi za awali ziondolewe. Ijapokuwa tumeitwa kuishi maisha ya haki, ambayo ni kwa kutii hizi amri, hatuwezi pata msamaha kwa kuanza kutii tu. Msamaha ni kipawa kunachopeanwa baada ya mtu; kuamini, kutii, kutubu, kubatizwa, na kupokea roho ya Mungu-waeb.6:1-2. Mungu unena wasiwasi kwamba, hawezi kumpa yeyote, roho yake, ikiwa huyu mtu hatii amri zake-War.5:32; waeb.5:9. Pia anahitaji mtu kushinda mpaka mwisho. Wokovu unategemea mtu kushikilia hiyo Imani mpaka mwisho wa maisha yake.**

2.Nilifikiria kwamba, agano la kale lilipita, kwa hivyo, hatuhitaji tena kutii hizo amri? JIBU: Hii inaelezwa katika nambari 2 pale juu. **Hii agano ilikuwa ni makubaliano waliyoyafanya waisraeli na Mungu pale Sinai. Hayo makubaliano ndiyo yalitupiliwa mbali baada ya Israeli kuyavunja, lakini ule msingi waliyojengwa juu yake ulibaki.Tukichunguza makubaliano ya agano jipya, tutagundua kwamba yamejengwa juu ya msingu huo huo, ambao agano la kale lilijengwa juu yake. Amri zile zile ambazo ndizo zilikuwa msingi wa agano la kale ndizo, zizo hizo ambazo juu yake, agano jipya limesimama-Jerem.31:31-33.** "Maana baada ya kupata makosa(ya watu, sio amri), anaahidi tena akisema, ' tazama siku zaja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na Juda: sio kama ile nilifanya na baba zao hapo nilipowatoa kwa nyumba ya utumwa kule Misri; maana hawakuendelea nayo, nami niliwakataa, asema Bwana. Lakini hili ndilo agano nitakalofanya nao, asema Mungu; **nitazitia amri zangu katika akili zao, na katika mioyo yao, nitaziandika:** Nami nitakuwa Mungu kwao, nao watakuwa watu wangu:"**Amri gani? Zingine mpya ama ni zile zile za mlima Sinai? Hapa ndipo ufahamu wa, ni nani aliyepeana amri pale mlima Sinai unahitajika. Mpeanaji wa amri katika agano la kale ni yeye yule ambaye anazipeana katika agano jipya. Kristo hakutupilia mbali, amri za baba yake. Ni yeye ambaye alizipeana pale Sinai. Ni yeye yule aliyehusiana na Musa uso kwa uso, ambaye Musa, Haruni na wale wazee sabini, walikula naye pale mlimani- Kutoka.33:1i,18; 34:6; 24:9-11.). Huyu waliomuona hakuwa Mungu baba mbali , Yesu. Hayo tunayafahamu kutoka- yohana 5:37; 1 Tim.6:16.Kwa hivyo, hili fikira la Yesu ambaye aliondoa amri za Mungu ni la uongo, na la kukozesha. Tofauti kati ya agano la kale na jipya ni mahali hizo amri zimewekwa. Kwa**

Waisraeli wakimwili, hizi amri ziliwekwa nje ya mioyo yao, kumaanisha, watu ambao hawajaongoka bado. Kwa wakristo, hizi amri zimewekwa, ndani ya mioyo, maana ya aliyeongoka. Kwa maelezo Zaidi, agiza, ujumbe wa, "hatuko chini ya sheria".

3.Kristo alikuja kutuletee amri mpya ya kupendana sisi kwa sisi-Yohana.13:34. Paulo anaonyesha wasiwasi kuwa, tukipendana, tunatimiza amri- War.13:10. Ikiwa tunawapenda wengine, basi tunatimiza sheria. Tunaishi katika pendo la Kristo naye anaishi ndani yetu. Kwa vile sasa tuko katika pumziko lake, basi hatuhitaji kutunza sabato, amri ya nne. Je wewe ukubaliani na hayo? JIBU: **Kunao upofu katika hii fikira. Yeyote ashikaye amri huwa na upendo kwa Mungu na pia kwa jirani- Mat.22:36-40. Upendo sio jambo jipya. Umekuwa ndani ya amri za Mungu tangu mwanzo(soma ujumbe katika tovuti ya www,endtimecog.org, uitwao, "Upendo ni aina ya maisha"). Ni kitu wayahudi hawakukielewa wala kukiona ndani ya hizo amri. Amri kumi ni maelezo ya upendo, na hivyo, upendo hauwezi kuziondoa. Hii hali ya kujaribu kuleta sababu ya kuziondoa ni jitihada la shetani kutoa watu kwenye maisha ya Mungu, maana pasipo hizi amri, upendo haujulikani. Tena, pasipo kuzitii, upendo hautimii.**
Angalia huu mfano. Nimeweka kibao barabarani kisemacho, " simama".Baada ya hapo, ninaendesha gari, halafu kufika kwa hicho kibao, nasimama.Hivyo, natimiza kile hicho kibao kinasema.Na kwasababu nimetimiza kile hicho kibao kinasema, sasa, hakuna mtu mwingine katika ya wale wanakubaliana nami, anahitajika kusimama, maana nimetimiza hilo agizo kikamilifu. Hivi ndivyo ukristo wa kisasa unavyofundisha. Hii namna ya kufikiria inakubalika kwa wale wanataka kuondoa sheria ya Mungu, wakiongea kuhusu uhaki wa Yesu(uliokuja kwa kuzitii amri za baba yake), huku wakiwa hawataki kufanya kama yeye.

4.Paulo alimaanisha nini aliposema, "Kristo ni mwisho wa sheria, kwa uhaki wa yeyote aaminiye-War.10:4?" JIBU: **Mtu anaweza kuuliza, " Wanafanya hayo kwa lengo gani?" Yaani, kwa kufanya ufanyavyo, unanuiya malengo gani? Basi malengo ya kutii sheria ni gani? Hili ndilo swali hasa, na jibu lake ni, ' kutunza sheria kunalenga kutufanya kuwa kama Kristo. Alizitunza sheria, sio? Wa-injilisti wanakubali kwamba alizitii vizuri sana, kiasi kwamba, hakuvunja ata moja(hakutenda dhambi), (ili aziondoe?), ndivyo wasemavyo. Makosa ya hilo fikira ni wasi, lakini lazima waendelee nalo ili waimarisha Imani yao, ya kukataa amri za Mungu ili wayashike mapokeo yao-Marko.7:9. Kama amri ziliondolewa, basi agano jipya imejengwa juu ya msingi gani? Na Kristo angekuwa na haja gani ya kuondoa amri ambazo yeye mwenyewe aliwapa wanadamu, Wa-israeli kwanza, halafu baadaye, wote watakaoshiriki agano naye?**
Tukisoma hiki kifungu na ilo akili la kupinga sheria, kinasema kitu moja kwetu. Tukikisoma na ile akili ya kutii amri, kinasema kitu tofauti. Ukweli ni kwamba, kinaeleza kile mtu huwa akimuiga Kristo, kwa kutii amri kama yeye. Eeee! Ile lengo la kutunza sheria ni ya mwishowe, tufanane na Kristo, yaani, vile alikuwa baada ya kutunza sheria, ndivyo tutakavyo kuwa baada ya kuzitunza- Mwisho wa sheria.
Kunao msimamo watu walijiwekea katika akili zao baada ya kudanganywa na shetani. Na kama vile Paulo anaeleza hapa, hii misimamo yao ni tofauti na ule yesu aliweka maana, "**Wakiwa hawajui haki ya Mungu, na huku wakitafuta kuimarisha haki yao wenyewe, hawakujitiisha katika haki ya Mungu-War.10:3".** Uhaki wa Mungu ni gani? Kuvunja amri zake? Hawa wayahudi walifikiria kwamba, kutunza sheria kulingana na vile walidhania zinapaswa kutunzwa, itatosha kuwaondolea dhambi. Hii ilichangia tu kuleta dini yao wenyewe, na sio uhaki wa Mungu- soma tena Yale majibu hapo juu, nambari.4.

5. Je, mtu anaweza kuokoka akikosa kutii mojawapo ya hizi amri, kama kwa mfano, kutotunza sabato? JIBU: **Tukisoma Yakubu.2:10, Mtu anaweza kudhania hili swali limejibiwa vibaya. Mat.5:19 inaeleweka vyena Zaidi, kuwa, hatuwezi kushika zile sehemu za amri tunapenda, huku tukiwacha zile hatupendi. Amri za Mungu ni maagizo makamilivu kuhusu vile tunapaswa kuishi. Ni jambo la wasi kwamba ile sheria ukristo wa siku hizi unataka kuondoa ni ile yenye kuonyesha umilele wa wakati. Amri ya Sabato uongea mambo ya wakati wa ile wiki ya uumbaji, kitambo kabla ya Sinai. Hiyo amri itatunzwa ata baada ya Kristo kuanzisha ufalme wake hapa duniani. Jambo la kuangalia ni kwamba, haya mabishano yote yanazunguka hiyo sheria ya sabato peke yake. Hakuna mtu uongea kuhusu kutupiliwa mbali kwa amri ya kuua, kusini, kutamani na zile zingine zote. Sasa tujiulize, kwanini tu, siku ya Mungu ya ibada peke yake, ndiyo wanataka kuondoa, na kuweka yao wenyewe ambayo haipatikani mahali popote katika maandiko?**
Sabato ilitunzwa na kanisa la kwanza la mitume. Historia na maandiko zinathibitisha hayo. Waeb.4: usema wasi kuwa……. " Utunzaji wa sabato bado upo kwa watu wa Mungu". Kristo atakaporudi, watu wote watarudi kutunza sabato ya Mungu-Isa.66:23.

Wako Ndugu katika Kristo,

Kabla hatujamalizia, hebu tuangalie vifungu vyenye maelezo Zaidi

Mat.5:17-18- "Msidhanie kwamba nalikuja kutangua torati au manabii. Sikuja kutangua ila, kutimiliza.Maana amini nawaambieni, 'ni rahisi mbingu na nchi kupita kuliko nukta moja la torati kutanguliwa". Wengi sana basi siku hizi, kinyume na Kristo, wanatangua, sio tu sehemu ndogo, mbali amri nzima kabisa.
War.3:20-21- "Basi, hakuna mwanadamu atakayehesabiwa haki kwa matendo ya sheria, maana kwa sheria uja ufahamu wa dhambi(sheria ueleza maana ya dhambi)". Lakini sasa, haki ya Mungu pasipo sheria imedhihirishwa, ikishuhudiwa na torati na manabii; (kwa hivyo hii sio fundisho jipya, kwani manabii na torati zinaishuhudia). Yaani, uhaki wa Mungu uliyo katika Imani ya Yesu, kwa wote waaminio: Maana hakuna tofauti: Maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; (dhambi inahuzisha watu wote ata wale wa agano, kumaanisha kuwa, sheria haikuja na hiyo agano, na hivyo, haikuondoka pia nayo). Kuhesabiwa haki bure kwa neema kupitia kwa ukombozi ulio ndani ya Kristo: ambaye Mungu amemfanya kuwa sadaka kwa Imani katika damu yake, kuonyesha uhaki wake kwa kuziondoa dhambi za awali, (Kuonyesha hitaji la damu, yaani kifo ata katika agano jipya), katika uvumilifu wake; , ili kutangaza uhaki wake: Ili aweze kuwa mwenye haki, na wakufanya kuwa haki, kila amwaminiye Kristo. Kuwapi basi kujisifu? Hakuna nafasi. Kwa sheria gani? Ya matendo? Hapana, lakini kwa sheria ya Imani. Kwa hivyo, tunasema kwamba, mtu uhesabiwa haki pasipo matendo ya sheria. Je, ni Mungu wa wayahudi pekee? Si wa wamataifa pia? Ndio, wa wamataifa pia: Basi kwa kuwa ni Mungu mmoja atakayewahesabia haki, wayahudi kwa Imani, ni yuyo huyo atakayewahesabia wamataifa kupitia kwa Imani. Basi je, tunaiwacha sheria kwa Imani? Hasha! Tunaitimiliza. (wahubiri, wakikozesha usemi wa Paulo wanamalizia kwa kuikataa sheria, kinyume na Paulo ambaye amemalizia kwa kuishikilia sheria, kuwa, Imani uhuzisha sheria kwa ile lengo lake la kiroho-War.8:4, Wakristo wa kweli hawavunji amri-War.6:14. " chini", umaanisha bado chini ya adhabu kwa kuvunja sheria. Aliyesamehewa utoka chini ya hiyo adhabu ya dhambi. Hawa

ujaribu kukozesha usemi wa Paulo, ili umaanishe kuwa, baada ya msamaha, mtu hapaswi tena kushika sheria(basi kumaanisha anapaswa kujiweka tena chini ya dhambi), badala ya kutokurudia dhambi tena).
1 pet.2:21-22- " Maana kwa hiyo pia nyinyi mliitwa:Maana Kristo yeye pia alitezeka kwa ajili yetu, akatuachia mfano ili tufuate nyayo zake: Ambaye hakutenda dhambi, wala hila kupatikana kinywani mwake: **Kutokufanya dhambi kunamaanisha kutii sheria(sio kwa niaba yetu, ila kama mfano wa vile tutafanya). Kama tunafuata nyayo zake, na huku hatutii sheria, basi hii inaachili kuwa, kwa vile tunafuata nyayo zake, basi yeye alikuwa muasi. Itawezekanaje tujiseme kufuata nyayo zake na tusitende kama alivyotenda? Yeye mwenyewe anatushangaa akiuliza, " kwanini mnaniita bwana Bwana, na hali hamyatendi niwaamuruyo-Luka6:46?"**
Wag.2:17- "Twajua ya kwamba, mtu ahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, lakini kwa Imani ya Kristo, ata tumemwamini kristo ili tuweze kuhesabiwa haki kwa Imani yake ni sio kwa matendo ya sheria: maana kwa matendo ya sheria, hakuna atakayehesabiwa haki. Lakini, ikiwa kwa kutafuta kuhesabiwa haki ndani ya Kristo, sisi wenyewe tunaonekana kuwa wenye dhambi, Kristo basi amekuwa mhudumu wa dhambi? Hasha! Unasikia? (Tunaelewa kuwa Yesu alizitii amri kikamilivu. Tukimkaribisha mioyoni mwetu, hivyo basi kusema anakaa ndani yetu, halafu tunavunja amri zile yeye alitii, basi tunaonyesha yeye ni muasi). Maana ikiwa tunarudia yale tuliwacha, basi sisi ni wenye makosa. Sasa niambie. Je, yesu ndiye sababu yako ya kutotii amri za Mungu? Eee, Yesu ni muasi?
1 Yohana.5:3- "Upendo wa Mungu ni kutii amri zake. Na amri zake sio nzito". **1yohana.2:3-7-** " Na twajua ya kuwa tunamjua ikiwa tunazishika amri zake. Yeye asemaye anamjua na wala azishiki amri zake ni muongo na kweli haimo ndani yake. Lakini yeye azishikaye amri zake, upendo wa Mungu umekamilika ndani yake:Na hivyo tunajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake imempasa kuenenda sawa sawa na vile alienenda. Wandugu, siwaandikia amri mpya, mbali ile ile mliokuwa nayo tangu mwanzo. Na hii amri ya zamani ni ile neno mlilolisikia tangu mwanzo. **Kunao uwasi ulio Zaidi ya huu? Kutii amri si njia ya kupata wokovu lakini, ni njia ya kuonyesha upendo kwa Mungu na wanadamu wenzako. Hapa hakuna furugu yeyote kuhusu kutii amri za Mungu maana ni wasi kuwa, ndizo maisha yake, na ya mwanadamu.**

Hayo yote tumeyasoma ni uthibitisho wa maana ya amri za Mungu maishani mwetu. Hili sio jambo geni kwa waaminio. Lakini maajenti wa Shetani tangu yadi, wanao njia ya ujanja ya kuondoa maana ya amri za Mungu , maana shetani anaelewa vizuri sana, mwanadamu asipojifunza kuishi kama zisemavyo hizo amri, atakufa.
Katika ujanja wake, Shetani utumia maandiko pia, ili kupumbaza wasio na ufahamu wa kutosha, ambao hawasomi biblia kuelewa kwa undani, inavyosema kuhusu kila hali ya maisha. Jiahdharini naye maana anao lengo la kuwafanya maadui wa Mungu msipokuwa waangalifu. Anawaonyesha vile Mungu ni mbaya, na vile anawanyima yale maisha ya furaha, kwa kuwaagiza mshike amri. Kwa vile huu mwili unapenda ukipingana na roho, utagundua kwamba, ni rahisi kushiriki tamaa za mwili kuliko kumtii Mungu-Wag.5:17. Kila mtu ambaye hajaongoka, hana roho ya Mungu, na kwa hivyo, hakuna vile anaweza kupenda na kutii hizo amri, maana ni uadui kwake. Yesu aliongea kuhusu viongozi wa wakati wake, akionyesha vile wanawafungia nje wafuasi wao kwa kuwafundisha uvunjaji sheria, huku

wakiwadanganya wanawaingiza ndani ya ukweli. " ole wenu nyinyi waandishi, wanafiki; maana mwafunga ufalme wa Mungu mbele za watu, maana nyinyi hamuingii na wala, hamwaachi wao kuingia. Ole wenu waandishi na mafarisayo, mwazibomoa nyumba za wajane, na kwa unafiki, mnafanya maombi marefu. Kwa hivyo, mtapata adhabu iliyo nzito Zaidi. Ole wenu waandishi na mafarizayo, maana mwaruka milima na bahari, kuwatafuta wafuasi, na mkimpata mmoja, mnamfanya kuwa mwana waupotevu mara dufu.-Mat.23:13-15. Mwana wa Jehanamu ni yupi? Inatupasa kumlika hilo. Hapa, wahubiri wanaenda mbali kumtafuta muumini, lakini wampatapo, wanamfundisha njia zao zilizo kinyume na mafundisho ya Mungu, na hivyo, wanaifanya vigumu zaidi kwa huyo muumini, kuamini ukweli kuliko wakati alikuwa hajawasikia. Mpaka wa leo, hawa waandishi na mafarisayo wako, na wana njia, kama vile tulivyoona, ya kuwadanganya watu, kuchukia amri za Mungu, ambazo ni maelezo ya maisha yake kwa mwanadamu.

Kila mtu anapenda upendo. Ni vile tu, wengi wanapenda ile ya msisimko wa moyo, na sio ile halisi itokanayo na matendo mema. Hawataki ile inayoingilia namna yetu ya kuishi kimwili, ile inahitaji tubadilishe namna yetu ya utendaji. Hii ndiyo sababu, hili fundisho la tupendane, bila mambo mengi, inapata kibali kwa wengi, maana ni, "sisimkeni tu, mfurahie, hiyo yatosha". Lakini ikiwa kweli tutamwamini Kristo, basi tukumbuke na kujua kwamba, alipeana masharti ya upendo, akisema, " mtu akinipenda, atazishika amri zangu-Yohana.14:15". Sio tu kwa uonyesho wa nje mbali, kama namna ya kuishi kutokana na moyo uliojawa hiyo akili, kama inavyoelekezwa na amri zake. Huu ndio upendo, ambao maajenti wa Shetani wanawazuia wote wawasikizao wasiufikie.
Kama wewe ni mwanafunzi wa hii njia ya ukweli, kama wewe ni kiongozi wa watu, Inakupasa Kuwa mwangalifu kuhusiana na, ile njia ya fikira unayotumia kama ufahamu. Naamini hili somo, litakupatia thibitisho la sababu yako ya kutunza amri za Mungu kama namna yako ya kuishi kila wakati. Mengi yapo katika hali ya kupotoka wakati huu, ambayo, ndio sababu Kristo anaamsha mioyo ya watu wake, wakumbuke sauti yake na kurudia ile njia ya milele-Amri zake. Tukumbuke kwamba, Kristo analikusanya kanisa lake sasa hivi, kutoka kwenye haya machafuko ya kiroho, ambayo yamefanya kanisa lake liwe fugufugu. Kama vile mithali ya wanawali kumi lionyeshavyo, kunao wakati wa kumaliza hii kazi, ambapo ukifika, wale hawatakuwa tayari watafungiwa nje. Kama umepewa kuisikia hii sauti, basi, usifanye moyo mugumu, maana hiyo siku yakaribia kwa mbio sana. Mwenye masikio na asikie vile Kristo analiambia kanisa

---------- **MWISHO**----------